

SABABU YA YESU KUJA VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA (MWALIMU)

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Kwanza

Africa Coordinated Curriculum for Bible Study

J2 — 1T

**Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI**

With permission of International Publications Services



Copyright, 1985
Baptist Publications House
All rights reserved

SABABU YA YESU KUJA

(MWALIMU)



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Kwanza

SABABU YA

YESU KUJA

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Pili

Kitabu cha Kwanza

YALIYOMO

Sura

Ukurasa

Ujumbe Kwa Mwalimu	5
1. Mwokozi Ambaye Mungu Aliahidi Kutuma	6
2. Yule Anayeelewa	11
3. Kazi ya Mwana wa Mungu	17
4. Yule Aliye Mkamilifu Pekee	23
5. Mwalimu Anayetoka Kwa Mungu	29
6. Wakati Tunapopinga Matendo Mabaya	35
7. Wakati Tunapohitaji Msamaha	40
8. Wakati wa Huzuni	45
9. Wakati Tunapopatwa na Mambo ya Ghafula	49
10. Njia ya Pekee Kwa Mungu	53
11. Njia Isiyopendwa	58
12. Ni Njia Ngumu Wakati Mwingine	64
13. Njia Imara	71

UJUMBE KWA MWALIMU

Jambo muhimu tutakalojifunza katika masomo ya kitabu hiki ni "Sababu ya Yesu Kuja." Jambo hili limegawanywa katika sehemu tatu: (1) Yesu ni Nani, (2) Yesu Aonyesha Jinsi Mungu Alivyo, na (3) Yesu Aonyesha Njia ya Kumwendea Mungu.

Kiini hasa cha Ukristo wetu ni ushirika wa kibinafsi na Kristo, kwa hivyo ni muhimu sisi kujua yale Biblia inafundisha kuhusu Yesu Kristo. Ni muhimu pia kwako wewe kama mwalimu kuwa na ushirika halizi na Kristo. Mfano wa maisha yako utakuwa sehemu muhimu sana ya ualimu wako. Maisha yako yatakuwa na mvuto zaidi kuliko maneno yo yote unayoweza kusema. Ukiwa na ushirika halisi na Kristo, vijana unaowafundisha wataweza kujifunza habari za Yesu kwa maisha yako.

Katika sehemu ya kwanza ya mafunzo haya, wanafunzi wako wataona ya kwamba Kristo ndiye masihi-mfalme wa unabii wa Agano la Kale, aliyekuja kuwa masihi-Mwokozi wetu. Wataimarika sana kiroho

wanapoona ya kwamba Kristo alifuata mpango wa Baba yake kwa ukamilifu; na kwamba ingawa alijaribiwa, alishinda; na kwamba yeye kama Mwalimu aliyetoka kwa Mungu, anaweza kuwaongoza kutii ukweli.

Katika sehemu ya pili ya kitabu hiki, wanafunzi watafikiria mambo manne kuhusu tabia ya Yesu. Wataona jinsi Yesu alivyofunua kikamilifu wema, huruma, msamaha, na uwezo wa Baba yake wa kusaidia. Wanafunzi wanapojua jinsi Yesu alivyotimiza mahitaji ya watu, wataona pia jinsi Mungu atakavyowatimizia mahitaji yao kama watamwamini.

Somo la mwisho la mafunzo haya linamdhihirisha Yesu kama Mwokozi. Na kwa vile Pasaka inakaribia, vijana watatumia wakati mwingi wakijifunza kusudi lililomfanya Yesu kuja.

Fanya juhudi maalum ya kujifunza masomo yako kwa uangalifu ili uweze kuwaongoza wanafunzi wako kufahamu vyema ya kuwa Yesu ni nani.

MWOKOZI AMBAYE MUNGU ALIAHIDI KUTUMA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 2:22-38

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Katika masomo ya kitabu hiki utakuwa na nafasi ya kuwaongoza wanafunzi wako kutambua mambo mapya kuhusu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Mambo hayo kuhusu Yesu ni nani yanaweza kuwa mvuto na kurekebisha maisha ya vijana wako. Katika kila somo, vijana wako watajifunza mambo fulani kuhusu Yesu ni nani. Labda utataka kuwasaidia wanafunzi kujua kwamba Yesu alikuja kama Mwokozi-Masihi ambaye Mungu aliahidi kutuma miaka mingi sana iliyopita. Wasaidie wanafunzi wako kuona kwamba Yesu ndiye Masihi na Mwokozi anayetuokoa katika dhambi.

Ukitaka kufahamu namna ya Masihi-Mfalme ambaye Wayahudi walimtumainia kuja, utahitaji kujifunza maandiko haya mengine: Yeremia 23:5-6; Mika 5:2; Isaya 7:14, 9:6-7, 53:4-6.

Kwa maandiko mengine katika Agano Jipya, utahitaji kusoma 1 Timotheo 1:15, Warumi 5:6-8, Ufunuo 11:15b, na Wafilipi 2:5-11. Maandiko haya yatakusaidia kueleza mambo ambayo Agano Jipya linafundisha juu ya Yesu, Mwokozi, aliyekuja kutuokoa katika dhambi.

Wakati unapofundisha usisahau kusudi la somo hili. Kusudi hilo ni kuwasaidia wanafunzi wako kufahamu kuwa Yesu Kristo aliyeshi miaka mingi

iliyopita ndiye Mwana wa Mungu aliyekuja kuwa Mwokozi kuwaokoa watu wote katika dhambi zao.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu alikuja kama Mwokozi-Masihi ambaye Mungu aliahidi kutuma.
2. Yesu hakuja kama Masihi-Mfalme kama taifa la Wayahudi walivyomtumainia.
3. Yesu alikuja kama Masihi-Mwokozi kutuokoa katika dhambi.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Sema): Na tujifanye siku ya leo kuwa tunasikiliza ripoti za mwandishi wa habari redioni ambaye aliulizwa kutoa ripoti ya siku maalum katika maisha ya jamaa ya kiyahudi Yerusalemu katika siku zile za Biblia. Lakini siku hii itakuwa muhimu zaidi kuliko vile alivyoitarajia kuwa. Hebu tusikilize sasa ambapo mwandishi huyo anaposema:

“Tuko ndani ya hekalu kuu la Herode ambapo hadithi yetu ya leo juu ya maisha katika Yerusalemu inapoanza. Tuna jamaa hapa ambao tutawatembelea leo. Jamaa hawa ni Mariamu na Yusufu seremala na Yesu mtoto wao. Jamaa hawa ambao ni wa mbari na jamaa ya Daudi wanatoka Nazareti ya Galilaya. Lakini hivi karibuni walikuwa wakikaa Bethlehemi. Wamekuja hapa kwa sherehe maalum inayofanywa baada ya mtoto kuzaliwa.”

"Mtu mmoja anasimama kusema nao. Naambiwa ya kwamba mtu huyu ni Simeoni, na kwamba ni mtu mcha Mungu. Namwona akimpokea mtoto Yesu mikononi mwake na anamshukuru Mungu. Na tusogee karibu sana naye ili tuweze kusikia mambo anayosema. 'Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, uliouweka tayari machoni pa watu wote; nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wote Israeli.' " (Luka 2:29-32).


"Simeoni anazungumza na Mariamu anayeonekana kuwa anastaajabu: 'Mtoto huyu atakua na kufanya maajabu mengi na mambo mema ya kuwasaidia watu. Mungu amemtuma ulimwenguni kuwa Mwokozi.' "

"Kweli jambo hili ni la kushangaza. Simeoni amesema ya kwamba mtoto huyu ni Kristo, mtiwa mafuta wa Mungu ambaye ni wokovu wa taifa la Israeli."

"Hapa tena kuna mtu mwingine. Mwanamke huyu mzee anayeitwa Ana, bila shaka ana umri wa miaka 100. Tangu mume wake alipokufa amekuwa akikaa hekaluni akimwabudu Mungu. Sasa yeye pia anambeba Yesu mikononi mwake na anamshukuru Mungu kwa mtoto huyu akisema ya kuwa mtoto huyu ni Masihi ambaye atakomboa taifa la Israeli."

"Je! Mariamu anafikiria nini baada ya kusikia mara mbili ya kwamba mtoto wake ndiye Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma?"

"Labda matangazo juu ya Masihi yatatangazwa hadharani hivi karibu. Na mpaka wakati huo, tunapaswa kuangalia kwa makini mambo yanayotendeka kuhusu mtoto huyu." (Mwisho wa ripoti ya mwandishi wa habari redioni).



Tunajua ya kwamba kuna unabii mwingi sana katika Agano la Kale unaosimulia habari za Masihi. Waalimu wa Kiyahudi walijifunza na kufundisha unabii huu, na baada ya miaka mingi waliendeleza wazo la kuonyesha mambo ambayo Masihi aliyeahidiwa angefanya.

Upanga na taji ni mifano ya vitu viwili ambavyo Wayahudi walimtumainia Masihi kufanya. (Uliza:) Je! vitu



hivi viwili vinakukumbusha nini? (Ndiyo, upanga unatukumbusha vita na ushindi juu ya maadui na taji inatukumbusha mfalme.) Wayahudi walitumainia kwamba Masihi angewashinda maadui za Israeli ili Israeli ingeweza kuwa tena taifa kubwa ulimwenguni. Pia walitumainia kwamba Masihi angeanzisha ufalme wake hapa duniani ambao ungetawala dunia yote hata milele. Walitumaini ya kwamba Masihi angerekebisha makosa yote kuwa sawa, kuhukumu haki, na kumletea kila mtu baraka. Walitumaini ya kwamba Masihi angefanya mambo haya yote kwa Wayahudi peke yao.

Kwa wazo lingine, Wayahudi walitumainia Yesu kuja kama Masihi-Mfalme. Lakini Agano Jipya linafundisha kwamba Yesu alikuwa Masihi-Mwokozi badala ya Masihi-Mfalme.

Msalaba na ulimwengu ni mifano ya mambo ambayo Agano Jipya linafundisha juu ya Yesu aliyekuwa Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma. (Uliza:) Je! picha hizi zinakukumbusha nini? (Msalaba unatukumbusha mauti na ulimwengu unatukumbusha watu wote.)



Yesu hakupigana vita na maadui za Israeli. Badala ya kuwafuata watu kumfanya kuwa mfalme wao,

aliwaruhusu watu kumsulibisha msalabani. Yesu alikuja kuokoa ulimwengu, si kuokoa taifa la Wayahudi peke yake. Hakuwa na taifa la Israeli peke yake katika mpango wake bali sisi sote tulikuwa katika mpango wake. Alikuwa kumpa kila mtu njia ya kusamehewa dhambi.

Tunaweza kuona kwamba Wayahudi walimfikiria Masihi kama Mfalme wa taifa lao, lakini Wakristo walijifunza kwamba Masihi alikuwa Mwokozi na Mfalme wa kila mtu binafsi ulimwenguni.

(Uliza:) Je! Simeoni aliyaelewa mambo haya kadiri gani?

Tunaposoma Luka 2:30-34, tunaona ya kwamba Simeoni alisema juu ya "wokovu". Waalimu wa Kiyahudi walikwisha kufundisha kwamba taifa la Israeli lingekolewa katika maovu ya maadui zake. Lakini Simeoni alifahamu ya kwamba wokovu wa Mungu maana yake ilikuwa ni kumwokoa kila mtu katika dhambi yake.

Pia, Simeoni alimwita mtoto Yesu, "Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa." Kila mtu ambaye si wa taifa la Wayahudi anajulikana Bibliani kama mtu wa Mataifa. Inaonekana kwamba Simeoni alifahamu wazi ya kwamba Yesu alikuwa Mwokozi wa watu wote wala si wa Wayahudi peke yao.

(Uliza:) Simeoni na Ana walimfahamuje mtoto Yesu? Roho Mtakatifu aliwafunulia mambo haya akilini na mioyoni mwao. Roho Mtakatifu anaweza kukusaidia kufahamu kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi ambaye Mungu aliahidi

kutuma miaka mingi sana iliyopita, na aliyekuja kukuokoa wewe katika dhambi na kuwa Mwokozi wako.

KAZI YA KUFANYA:

(Tumia wakati huu kufundisha pia. Utakapotembea chumbani, wasaidie wanafunzi kuandika majibu mazuri ya maswali.)

Hapa kuna majibu ya sehemu ya “Kazi ya Kufanya” katika vitabu vya watoto.

Wayahudi walimtazamia Masihi au Kristo kuja. Walipata maelezo katika Agano la Kale yaliyowaeleza jinsi Masihi angekuwa na mambo ambayo angefanya. Soma vifungu vichache kati ya vifungu vinavyoeleza mambo ambayo Mungu alisema kuhusu Masihi.

Soma Yeremia 23:5, 6 na upige mistari chini ya maneno yanayoeleza jinsi Masihi angekuwa.

Mshauri wa kisiasa.

Mwenye haki.

Mfalme.


Askari.

Mwenye kuhukumu na haki katika njia zake zote.

Mkuu wa Mji.

Mlinzi wa Yuda na Israeli.

Soma Mika 5:2 kisha uchore mwingo kwa jina la mji ambapo Mwokozi angezaliwa.



Soma Isaya 9:6, 7 na Zekaria 9:9, 10 halafu jibu maswali haya.

Je! ufalme wa Masihi ungedumu kwa muda gani? hata milele.

Je! Masihi angetawala kuanzia wapi mpaka wapi ulimwenguni? toka bahari hata bahari, na toka mto hata miisho ya dunia.

Fungua Agano Jipya sasa upate maelezo juu ya Yesu Kristo ambaye alizaliwa Bethlehemu.

Soma 1 Timotheo 1:15 na Warumi 6:6-8 na uandike jibu la swali hili.

Je! Yesu alikuja kufanya nini hapa ulimwenguni? Awaokoe wenye dhambi.

Soma Ufunuo 11:15b na uandike jibu la swali hili.

Je! Yesu atatawala ufalme wa dunia kama mfalme? Ndiyo.

Soma Wafilipi 2:5-11 na uandike namba 1 kando ya maneno yanayoeleza jinsi Kristo alivyokuja ulimwenguni kwa mara ya kwanza. Andika namba 2 kando ya maneno yanayoeleza jinsi Kristo atakavyoonekana siku nyingine.

- 1 bila heshima
- 1 mauti
- 1 utumishi
- 2 cheo kikuu
- 2 Bwana

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu.”

Yohana 6:69

Taifa la Wayahudi lilimtumainia Yesu kuja kama Masihi-Mfalme ambaye angewaokoa na maadui zao. Lakini Yesu alikuja kama Masihi-Mwokozi kuwaokoa watu wote katika dhambi zao.

Kila mtu hakumtambua Yesu wakati alipokuja. Hata sasa watu wengine hawamjui Yesu. Watu wengine humfikiria Yesu kuwa ni mtu mwema tu aliyeshi miaka mingi sana iliyopita. Wengine bado wanamngojea kuja.

Watu wengine wanamjua Yesu kama Mwokozi na wanatazamia wakati atakapotawala kama Mfalme. Wanafunzi wa Kristo wangesema maneno ya kifungu hicho cha kukumbuka kwa hakika. Wasaidie wanafunzi wako kujua ukweli wa maneno hayo. Labda wao pia wanaweza kusema maneno hayo kwa hakika.

WAKATI WA KUFUNGA:

Labda utapenda kufunga mafunzo kwa kuomba maombi ya kumsifu Mungu kwa kumtuma Yesu kuwa Masihi na Mwokozi wetu.

(Sema) Wakati Roho Mtakatifu alipomwongoza Simeoni kwenda hekaluni ambako mtoto Yesu alikuwamo, na alipomwonyesha Simeoni ya kwamba Yesu alikuwa Kristo na Mwokozi ambaye Mungu aliahidi kutuma, Simeoni aliomba ombi la sifa ambalo lilikuwa kama zaburi au wimbo. Ni mojawapo ya nyimbo chache zilizo ndani ya Agano Jipya.

(Sema) Sisi pia tunaweza kuomba maombi mafupi ya sifa ya kuonyesha mawazo yetu juu ya Yesu ambaye ni Kristo. (Wasaidie wanafunzi wako kufikiria sababu ya wao kufurahi leo kwamba Yesu alikuja. Kisha omba maombi ya kumsifu Mungu kwa kumtuma Mwanawe, Yesu Kristo kuwa Mwokozi wa ulimwengu.)

YULE ANAYEELEWA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 2:39-52
KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Jambo unaloweza kuwasaidia wanafunzi wako kutambua ni kwamba Yesu ndiye anayewaelewa kamili. Mungu alimtuma Yesu ulimwenguni katika mwili wa mwanadamu ili angeweza kukua kama vijana wanavyokua na kuwafariji katika hali yao ya kukua.

Bila shaka, wanafunzi wako mara kwa mara hufikiri kwamba watu wazima hawawafahamu wala hawawajali. Ni vigumu zaidi kwa vijana wako kufikiria kwamba Kristo tunayemwabudu, pia alikuwa mtoto kama wao walivyokuwa watoto. Ni ajabu kumfikiria Yesu kwamba alikuwa kijana hasa.

Wanafunzi wako wanahitaji kujua kwamba Yesu alikuwa mwanadamu ikiwa wanataka kujua kwamba Yesu anawafahamu kadiri gani. Yesu pia alikuwa mdogo na alikabili mambo kama ya kwenda shuleni kujifunza, kusaidia kazi nyumbani, na kutii sheria za wazazi wake. Yeye ndiye anayefahamu furaha na huzuni ya vijana wako. Na yeye ndiye Mwana wa Mungu anayeshughulikia maisha ya watoto wake, na anayetaka kuwafariji na kuwatumia katika kuwasaidia na kuwafariji wengine.

Ili kuwasaidia vijana wako kufahamu mpango wa Mungu wa kutoa faraja na ufahamu, itakubidi kujifunza maandiko haya mengine. Waebrania 2:18; 1 Petro 5:7; Zaburi 86:15; Kumbu-

kumbu la Torati 8:2a, Wagalatia 6:2; na 2 Wakorintho 1:4.


Wakati unapofundisha, *kusudia kuwafundisha wanafunzi wako kwamba Mungu alimtuma Yesu ulimwenguni kama mwanadamu ili kuwafahamu na kuwafariji*. Wasaidie kutumia njia ya Mungu ya kutoa faraja na ufahamu ili kujisaidia wao wenyewe na kuwasaidia wengine.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Mungu alimtuma Yesu, Mwanawe, ulimwenguni kama mwanadamu, akakua kama watu wote wanavyokua.
2. Unaweza kufarijiwa kujua kwamba Yesu anafahamu kamili hali unayokabili na jinsi unavyowaza moyoni mwako wakati huu ambapo unakua.
3. Mungu hutoa faraja na ufahamu katika njia nyingi.
4. Mungu hutumia watu wengine kutufariji na kutusaidia, na hututua sisi pia kuwafariji na kuwasaidia wengine wanaohitaji ufahamu.

KULIFUNDISHA SOMO:

Wakati Yesu alipokuja duniani aliishi kama watu wengine walivyoishi. Kabla ya kuja kwake duniani hakuwa na mwili kama wetu, Lakini kwa sababu ya kuja duniani, alitwaa mwili wa mwanadamu, akawa mmoja wetu. Alizaliwa kama mtoto mchanga, kama wewe ulivyojaliwa. Alikua kama unavyokua, akawa mtu mzima.



(Uliza:) Je! kwa nini Mungu alimpangia hivyo? Kwa nini Mungu hakumtuma Yesu duniani kama mtu mzima? Kwa vile Yesu ni Mwana wa Mungu na Masihi aliyehidiwa kuja, mbona hakuishi maisha tofauti na yetu? Unafikiri kwamba ilimbidi Yesu kufanya uchaguo wo wote? Je! alikuwa na taabu kama zetu?


(Sema:) Somo letu la leo litatusaidia kujua majibu ya maswali hayo.

Katika somo lililopita tulizungumza juu ya Simeoni na Ana walipowaona Yesu na wazazi wake hekaluni. Baadaye Mariamu na Yusufu walimpeleka mtoto Yesu Bethlehemu na walikaa huko mpaka malaika wa Mungu alipomwonya Yusufu katika ndoto ya kwamba mfalme Herode alikuwa akimtafuta mtoto Yesu kumwua. Jamaa hawa walikimbilia nchi ya Misri na walikaa huko mpaka mfalme Herode alipokufa. Kisha ndipo walirudi Nazareti, mjini kwao.

Yesu alikua katika mji huo wa Nazareti. Tunaweza kusoma juu ya utoto wake katika Luka 2:39-40, 52.

(Uliza:) Je! ilimpasa Yesu kwenda shuleni kama wewe unavyofanya? Ndiyo, ilimpasa kufanya hivyo. Watoto nyakati zile walianza kwenda shuleni walipokuwa na umri wa miaka mitano

au sita na kuendelea mpaka walipotimiza umri wa miaka kumi.




(Uliza:) Je! Yesu alicheza michezo ya namna gani? Je! alishinda katika michezo kila siku kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu? Je! alijaribu kudanganya hata siku moja? Watoto wa nyakati zile ambao ni kama wa sasa, walicheza mpira na kukimbia mbio. Kwa sababu Yesu alikua kama watoto wengine wanavyokua, pengine alifurahia michezo. Lakini hakushinda kila siku eti kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu. Tunajua ya kwamba hakudanganya kwa sababu yeye akiwa kama Mwana wa Mungu alifanya mambo yaliyo haki peke yake.

(Uliza:) Je! kwa sababu Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, ilimpasa kufanya kazi yo yote nyumbani mwao? Mungu alimchagulia Mwanawe kuzaliwa katika jamaa maskini. Kazi ilikuwa ikitendwa na wanaume na wanawake. Lakini kwa hakika ilikuwa muhimu kwa Yesu kusaidia kwa kazi ya wanaume.

(Uliza:) Je! Yesu alifikiri kama ninyi kuhusu mambo ambayo angefanya wakati ambapo angekuwa mtu mzima? Wavulana katika siku zile za Yesu walifundishwa kazi ambayo

wangefanya kama tunavyofanya siku hizi. Kila mvulana alijifunza kazi fulani, lakini hasa ile ambayo baba yake alifanya. Labda Yesu alijifunza kazi ya useremala kwa maana Yusufu baba yake (mlezi) alikuwa seremala. Bila shaka Yesu alitengeneza vitu kama majembe (ya ng'ombe) ya miti, nira, meza ndogo, viti, na masanduku.



(Uliza:) Je! ilimpasa Yesu kuwatii wazazi wake kama ninyi mnavyofanya ingawa alikuwa Mwana hasa wa Mungu? Tuna hadithi moja katika Biblia inayotupa jibu. Hebu tuone jambo lililomfanyikia Yesu wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili.

Hatimaye Yesu alikuwa mkubwa wa kutosha kujiunga na wasafiri kwenda katika hekalu kuu Yerusalemu kuadhimisha sikukuu ya Pasaka. Jamaa ya Yesu walijitayarisha kwa safari katika mwezi wa Aprili. Siku moja asubuhi wakati kila kitu cha safari kilipokuwa tayari, Yesu alikwenda pamoja na mama yake na Yusufu kwenye mlango wa mji wao. Watu wengi walikuwa wamekusanyika pale ili kusafiri pamoja kwenda hekaluni Yerusalemu. Kundi hilo la watu walisafiri siku kadha. Katika siku ya mwisho wakati walipokaribia Yerusalemu, Yesu alianza kutazama hekalu kwa mara ya kwanza. Alipoona mawe yake yaliyometameta kwa mbali, yeye pamoja na vijana wengine waliimba nyimbo za kumsifu Mungu.

Mwishowe walifika katika mlango wa mji wa Yerusalemu. Walitembea mjini humo na hatimaye wakaingia hekaluni. Sikukuu ya Pasaka ilichukua wiki moja na siku moja (yaani, siku nane). Kila siku wakati Yesu alipokuwa Yerusalemu alikwenda hekaluni. Aliomba, aliimba nyimbo, na aliwasikiliza waalimu wakisoma Neno la Mungu.

Alijiunga na makundi madogo ya watu waliokusanyika katika vyumba ya hekalu kusoma na kuzungumza juu ya maandiko pamoja na waalimu. Yesu aliwauliza waalimu maswali mengi sana. Wao pia walimwuliza maswali naye aliwapa majibu yaliyowashangaza.

Baada ya ibada za hekalu kumalizika, (yaani mwisho wa wiki ile ya sikukuu ya Pasaka), Mariamu na Yusufu walianza safari ya kurudi nyumbani kwao Nazareti. Walikuwa na wasiwasi sana wakati walipotambua ya kwamba Yesu hakuwapo pamoja nao. Siku mbili zilikuwa zimepita tangu walipomwona Yesu. Je! Yesu alikuwa wapi? Waliporejea Yerusalemu, walimtafuta kila mahali.

Mwishowe walimkuta hekaluni. Bila shaka Mariamu alimwona Yesu

akimtazama, akamwita kwa kumpungia mkono. Alimwuliza Yesu kwa wasiwasi, "Mwanangu, mbona umetutenda hivi?" Yesu alimjibu, "Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" (Luka 2:49) Yesu alikuwa na maana kwamba iliwapasa wazazi kujua kwamba yeye kama Mwana wa Mungu, angenda kujifunza kwa waalimu wale maandiko juu ya Mungu, Baba yake.

Lakini Mariamu na Yusufu bado hawakuelewa kamili mambo ambayo Yesu alikuwa akiwaambia.

Yesu ambaye alikuwa Masihi na Mwokozi aliyengojewa kwa miaka mingi kuja, alirudi Nazareti pamoja na Mariamu na Yusufu na aliwatii wazazi hawa wake walezi katika miaka yake yote ya kukua. Siku moja, wazazi hawa wake na ulimwengu wangejua kweli ya kwamba yeye alikuwa nani.

(Rudia maswali uliyouliza katika mwanzo wa somo hili.)

(Uliza:) Je! kwa nini Yesu alikuja duniani kama mtoto mchanga badala ya kuja kama mtu mzima? Je! ilimbidi Yesu kufanya uchaguo kama inavyotupasa sisi? Je! alikuwa na taabu kama zetu?

(Sema:) Kifungu chetu cha kukun.ouka kinatupa wazo la kutupa majibu. Na tusome pamoja. (Wakati huo ndio utafaa sana kufundisha kifungu cha kukumbuka. 2 Wakorintho 1:3, 4a)

Mungu ni Baba anayetaka kutufariji wakati tuna huzuni au tunapokuwa na

taabu au mahitaji. (Uliza:) Mungu hutupaje faraja? Njia moja ambayo Mungu hutufariji wakati tuna huzuni au tuna taabu ni kutuhakikishia kwamba kuna mtu anayefahamu hali zetu. Kwa ajili hiyo, alipanga ya kwamba Yesu angekua kama unavyokua ili angeweza kufahamu jinsi unavyowaza. Tunafarijiwa tunapojua ya kwamba wakati Yesu alipokuwa akikua alikuwa na mawazo kama yetu tunapokua.

Yesu anaweza kufahamu majaribu yetu kwa sababu yeye pia alijaribiwa. Kwa sababu Yesu hutujalia sisi, tunaweza kumpelekea taabu zetu zote au kushiriki taabu hizo naye.

Njia nyingine ambayo Mungu hutufariji ni kutusaidia kukumbuka ya kwamba yeye ni Mungu mwenye huruma. Kuwa na huruma maana yake ni kujua taabu za mtu na kumfanyia jambo la kumsaidia. Tunasoma katika Biblia jinsi Mungu alivyofanya hivyo kwa watu wake mara kwa mara. Hutufanyia sisi pia.

Mungu anataka tukumbuke wema wake kwetu. Wakati mwingine inakuwa msaada kwetu kukumbuka kifungu kama hiki chetu cha kukumbuka. (Rudia kifungu hicho tena.) Wakati mwingine tunaweza kukumbuka hali tuliyokuwa nayo ambayo kwayo Mungu alitupa msaada na faraja yake. Hii itatusaidia kumwamini kutupa faraja tunayohitaji sasa.

Njia nyingine ambayo Mungu anaweza kutuhakikishia juu ya faraja yake ni kwa watu. Mungu hutumia watu wengine kutusaidia, na hututumia

sisi pia kuwasaidia watu wengine. Mungu anatwambia kushiriki na wengine katika taabu zao kwa kutweka mizigo ya taabu hizo zao pamoja nao. Maana yake sisi kumbebea mtu mwingine mzigo wake mzito, lakini ni kufariji roho ya mtu iliyo na huzuni ili aweze kuwa na furaha tena. Sisi hushiriki na mtu wakati tunaposikiliza na kujaribu kufahamu taabu yake, na wakati tunapokumbuka kumwomba.

KAZI YA KUFANYA:

Jaza maneno yanayokosekana katika sentensi zifuatazo:

Soma Waebrania 2:18

Kristo anaweza kufahamu majaribu yetu kwa sababu yeye pia alijaribiwa.

Soma 1 Petro 5:7

Kwa maana Kristo hujishughulisha kwa mambo yetu, tunaweza kumtwika yeye fadhaa zetu zote.

Soma Zaburi 86:15.

Tunajua ya kwamba Mungu hutufahamu kwa sababu yeye ni Mungu wa rehema na neema.

Soma Kumbukumbu la Torati 8:2a.

Mungu anatwambia kuikumbuka njia ile aliyotusaidia zamani.

Soma Wagalatia 6:2

Ili kutusaidia kuwaelewa watu wengine, Kristo anatwamuru kuchukua mizigo yao.

Soma 2 Wakorintho 1:4

Kwa sababu Mungu hutufariji katika dhiki zetu, sisi pia twapaswa kuwafariji wale walio katika dhiki.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote."

2 Wakorintho 1:3,4a

Mapendekezo kuhusu kufundisha maana ya vifungu hivi na matumizi yao yanapatikana katika sehemu ya "Kulifundisha Somo."

WAKATI WA KUFUNGA:

Tumejifunza kwamba Mungu hutufariji kwa kutumia watu wengine. Hutumia watu wengine kutusaidia na hutumia sisi kuwasaidia watu wengine. Kwa sababu Mungu hutufariji katika taabu zetu, inatupasa sisi pia kufarijiana.

Je! baada ya Mungu kutufariji, hutaka sisi kufanya nini? (Hutaka sisi kuwasaidia watu wengine kwa kuwaonyesha kwamba tunafahamu taabu yao na kwamba tunawajali.)

Fikiria mtu fulani anayehitaji kukumbukwa, mtu fulani aliye na taabu, ambaye ni mgonjwa, aliye na wasiwasi juu ya pesa, au shule, mtu fulani aliye pekee au aliye na mahitaji. Wafikirie jamaa yako, waalimu, marafiki, na majirani.

(Uliza:) Je! unaweza kufanya nini ili kufariji? (Zungumza na wanafunzi kuhusu mambo wanayoweza kusema kama, "Nafahamu," au "Nasikitika..." au "Napenda kusaidia," au "Najali." Wasaidie vijana kufikiria jambo wanaloweza kuwafanyia watu wengine ambalo linaweza kuwaonyesha kwamba wanafahamu taabu yao na

kujali na kutaka kuwafariji kama Yesu alivyowafariji.)

(Sema:) Kata shauri juu ya mtu mmoja utakayejaribu kumfariji katika njia maalum na kuwa tayari kueleza jinsi ulivyomfariji katika somo lijalo. (Funga darasa kwa maombi ukimshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu anayetufahamu na kutufariji. Pia, waombee watu ambao wanafunzi watajaribu kuwafariji.)

KAZI YA MWANA WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana
1:1-34; Mathayo 3:13-17

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Ingawa vijana unaowafundisha wanapendelea mambo yanayotukia maishani mwao sasa, kuna wakati ambapo wao hufikiria siku zao za baadaye. Ingawa ni wadogo, wanaanza kuona ya kwamba wana tamaa na uwezo maalum ambao unaweza kuwa na mvuto kwa hali watakayokuwa nayo na kwa mambo watakayofanya wakiwa kama watu wazima.

Wakati huu sio mapema bali ndio wakati unaowapasa vijana wako kujifunza kwamba Mungu ana mpango au kusudi kwa maisha yao. Huu ndio wakati unaompasa kila kijana kutumia akili yake kutambua mpango wa Mungu kwa maisha yake, na kutoa kitu cho chote chake na kujitoa mwenyewe kwa matumizi ya Mungu.

Yesu alifanya hivyo. Somo hili linafundisha kwamba Yesu, Mwana wa Mungu alitwaa mwili wa mwanadamu ili kuweza kutimiza kazi yake ya kuwaokoa watu katika dhambi zao. Yesu alikuwa mtiifu kamili kwa kazi yake kama Mwana wa Mungu.

Ili kujitayarisha mwenyewe kuwasaidia wanafunzi wako kufahamu ukweli wa somo hili, ujifunze Yohana 1:1-14 kwa uangalifu. Maandiko haya ndio msingi wa sehemu ya "Kazi ya Kufanya" katika vitabu vya vijana.

Kusudi la somo hili ni kuwaongoza wanafunzi wako kujua kwamba Yesu alijitoe kamili kwa kazi yake ya kuuokoa ulimwengu ili wanafunzi hao wataweza kujifikiria mwito wao binafsi kwa Yesu na pengine watapenda kutoa maisha yao kwa utumishi wake.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu alikuwa mtu maalum, alikuwa Masihi aliyekuwa na kazi maalum ya kufanya.
2. Yesu, Mwana wa Mungu alikuwa ulimwenguni katika mwili wa mwanadamu.
3. Wakati alipobatizwa, alijitoe mwenyewe kwa kazi maalum ya kuwaokoa watu katika dhambi zao.
4. Tunaweza kujitoe sisi wenyewe kwa kazi ya Mungu ili kuwa kama anavyotaka na kutenda mambo anayotwambia.

KULIFUNDISHA SOMO:

Wakati Yesu alipokuwa akikua alikabili taabu za kila siku kama zetu. Lakini wakati ulifika ambapo ilimbidi kuacha mambo yote na kufanya juhudi kamili ya kutimiza kazi ambayo Mungu alimtuma kuja kufanya.

Katika somo lililopita tulijifunza kuhusu wakati ambapo Yesu alikwenda hekaluni Yerusalemu alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili. (Uliza:) Je! Yesu alifanya nini baada ya kurejea Nazareti? Katika Luka 2:51,52

tunasoma ya kwamba “Akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii; na mamaye aliyaweka hayo yote moyoni mwake. Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” Ingawa hatujui jambo lote Yesu alilosema au alilofanya kwa miaka 18 katika umri kati ya umri wa miaka 12 na 30, bila shaka alijua zaidi ya kwamba alikuwa mtu maalum na Masihi aliyekuwa na kazi maalum ya kufanya.

(Uliza:) Je! kazi yake maalum ilikuwa nini? Tutajaribu kupata katika somo hili jinsi ulimwengu ulivyomtambua Yesu na kazi iliyompasa kufanya.

Katika ukingo wa Mto wa Yordani katika nchi ya Uyahudi, palisimama mtu mmoja kuwaelekea mkutano wa watu. Mtu huyo alivaa vazi la singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake. Nywele zake zilikuwa ndefu. Njia zake za maisha zilikuwa za kimaskini na maneno yake yalikuwa ya haki. Ilisemekana kwamba chakula chake kilikuwa asali ya mwitu na nzige.



“Je! ni nani huyo anayehubiri?” mtu mmoja aliuliza.

“Ni Yohana,” mtu mwingine alimjibu. “Yeye ni mwana wa kuhani mmoja wa hekalu. Anaitwa Yohana Mbatizaji kwa sababu anawabatiza watu.”

“Je! anahubiri juu ya nani?”

“Sikiliza, nawe utajua. Yuko tayari kuhubiri.”

Watu walisogea mbele na Yohana Mbatizaji akaanza mahubiri yake.

“Ni lazima mtubu,” alisema. “Ni lazima mgeuze nia zenu juu ya mambo mabaya mnayotenda na kuacha mambo hayo. Ni lazima mtende haki. Mungu anaweza kuwasamehe dhambi kama mkiacha dhambi zenu. ‘Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.’ ” Watu wengi waliacha njia zao mbaya wakabatizwa.

“Je! mhubiri ni Kristo, Masihi ambaye Mungu aliahidi kutuma?” watu waliuliza. Yohana Mbatizaji alisikia swali hilo lao, akatikisa kichwa chake. “Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu.” (Marko 1:8) Aliwaeleza mkutano ule wa watu kwamba, “Baada ya siku chache kutakuja mtu nyuma yangu mwenye nguvu kuliko mimi. Sistahili kuvichukua viatu vyake. Atakapokuja ataondoa maovu mioyoni mwenu kama moto unaoteketeza makapi. Atawamwagieni Roho Mtakatifu kama maji ya ubatizo unaowafunikiza.” Yohana alikaza kwamba njia iliyokuwa nzuri ya kujitayarisha kwa kuja kwa Masihi ilikuwa ni kujisikitisha kwa ajili ya dhambi zao na kubatizwa. Ubatizo

ulikuwa thibitisho la hadhara ya kwamba mtu alitubu dhambi zake na kwamba sasa alitaka kuishi maisha ambayo yangempendeza Mungu.

Siku moja, wakati Yohana alipokuwa akihubiri, alimwona mtu mmoja aliyekuwa akimjia na kumwuliza kumbatiza.

“Mtu huyu ni seremala kutoka Nazareti,” mtu mmoja alinong’oneza. “Anaitwa Yesu.”

Labda watu wengine walistaajabu, wakisema, “Mhubiri atamwambia mtu huyu kufanya nini?”

Kisha walimwona Yohana Mbatizaji akitikisa kichwa chake kama ishara ya kukataa. Walimsikia akisema lakini hakumwambia Yesu kutubu wala kufanya jambo lo lote. Yohana alistaajabu kwamba Masihi alikuja kwake kutaka kubatizwa. Alimwambia, “Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?”

Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote.” (Mathayo 3:14b-15a).

Yohana hakushindana naye tena. Alimwongoza Yesu wa Nazareti kuingia majini katika Mto wa Yordani, akambatiza. Wakati Yesu alipopanda kutoka majini, alitazama juu mbinguni, akasimama kimya katika maombi. “Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake, na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu,

ninayependezwa naye.' " (Mathayo 3:16-17).



Huyu ni mwanangu,
mpendwa wangu,
ninayependezwa naye.

Mara Yohana alikumbuka ahadi ya Mungu ambayo Mungu alikwisha kumwahidi miezi kadha mbeleni. Ahadi hiyo ilisema, "Utamjua Mwanangu wakati utakapomwona Roho wa Mungu akishuka juu yake." (Soma Yohana 1:33-34) Yohana Mbatizaji alikwisha kuona mwanga. Alikwisha kuisikia sauti ya Mungu akimthibitisha Yesu kama Mwanawe na kuthibitisha ubatizo wake.

"Kweli, huyu ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai," Yohana alisema. Wakati huu ulikuwa wakati mkuu kwa Yesu na kwa Yohana. Kutokea wakati huu ndipo Yesu Mwana wa Mungu angefundisha na kuhubiri Neno la Mungu. Kutokea wakati huu pia ndipo Yohana angeweza kudhihirisha Yesu kama Mwana wa Mungu na kusema kwa hakika kwamba, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." (Yohana 1:29) Yesu, Mwana wa Mungu, alikuwa ameanza kazi yake.

Tunajua ya kwamba Yesu alipokuja ulimwenguni kutoka mbinguni, alikuja katika mwili wa mwanadamu, akawa kama sisi. (Uliza:) Kwa nini Yesu, Mwana wa Mungu alikubali kuja ulimwenguni katika mwili kama wetu? Yohana Mbatizaji alisema kwamba Yesu "huichukua dhambi ya ulimwengu." Yesu aliwakubalia watu ambao hawakumwamini kama Mwana wa Mungu kumsulibisha msalabani. Wakati Yesu alipokufa, alichukua lawama za dhambi ya kila mtu na aliadhibiwa kwa ajili yetu. Hakuadhibiwa kwa sababu ya dhambi zake mwenyewe. Lakini kila mtu ulimwenguni ametenda dhambi. "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." (Warumi 3:23)

Tukikubali kwamba tumetenda dhambi, na kuamini kwamba Yesu aliondoa lawama ya dhambi zetu kwa kufa msalabani, basi Mungu atatusamehe dhambi zetu.

Tunaambiwa wazi katika kifungu cha kukumbuka kazi ya Mwana wa Mungu. (Huu ndio wakati mzuri kufundisha kifungu cha kukumbuka.) Someni Yohana 3:16-17 pamoja. Kisha sema: Yesu alikuwa mtiifu kamili kwa kazi ambayo Mungu alimtaka kufanya. Mungu alionyesha kwamba alithibitisha kazi hiyo yake kwa kumtuma Roho Mtakatifu kumtia Yesu nguvu ya kuendelea na kazi yake.

Wakati Yesu alipobatizwa, alijitoa mwenyewe kwa utumishi maalum. Hakuwa akitubu dhambi, bali alikuwa akiomba mapenzi ya Mungu kufanyika, na alikuwa akimfahamisha Mungu kwamba alikuwa tayari na

alikuwa na nia ya kutenda kazi ya Mungu katika njia ya Mungu mwenyewe.

(Sema:) Ingawa hatujui hasa jambo ambalo Mungu anatutaka sisi kuwa au kufanya wakati tunapokua, tunaweza kuamua sasa kuwa kama Mungu anavyotaka. Tunaweza kuwa na hakika kwamba Mungu anajua jambo lililo jema kwetu kufuata, na linalotupasa kufanya. Anatumulisha jambo hilo katika wakati unaofaa.

Unaweza kutoa maisha yako kwa Mungu hata sasa kwa kumwambia ya kwamba uko tayari kuwa katika hali anayokutaka na kufanya kama anavyotaka.


(Ukipenda unaweza kuwa na muda mfupi wa maombi ya kimya ambapo kila mwanafunzi anaweza kuomba kwa juhudi hasa maombi ya kujitoa kwa utumishi wa Mungu.)

KAZI YA KUFANYA:

Yesu alikuwa mtu maalum aliyekuwa na kazi maalum ya kufanya. Alikuwa kweli Mwana wa Mungu. Anaitwa Neno la Mungu aliye Hai kwa sababu alikuwa Mungu aishiye miongoni mwa watu. Unaposoma vifungu vifuatavyo, utapata mambo mengine muhimu juu ya kazi ya Yesu hapa ulimwenguni.


Soma vifungu vya Biblia na kuandika vizuri maneno yafuatayo.

Soma



NONE (NENO) alikuwako kwa Mungu tangu mwanzo. Vyote vilifanyika kwa **YOHU (HUYO)**.

Soma




NINDA (NDANI) yake ndimo ulimokuwamo uzima. Nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu wote.

Soma




Mungu alimtumia Yohana Mbatizaji kuhubiri habari za mtu huyu, lakini Yohana hakuwa mtu **LEYU (YULE)**.

Soma




Angalia ya kwamba "NURU" ni jina lingine la mtu huyu anayeitwa Neno. Nuru alikuwako ulimwenguni, na ulimwengu **HAUKUTAAMBUM (HAUKUMTAMBUA)** yeye.

Soma



Neno, ambaye pia ni Nuru, alikuja ulimwenguni na kukaa TIKA (KATI) ya watu wale, lakini wao hawakumpokea. Lakini LEWA (WALE) waliompokea kwa kumwamini yeye wanaweza kuwa wana wa Mungu.

Soma



Tukimpokea Neno ambaye pia ni Nuru, tunazaliwa mara ya pili kwa Mungu, wala hatuzaliwi kwa uwezo wetu sisi WEWENYE (WENYEWE).

Neno mwenyewe alifanyika mwili, AKAATA (AKAKAA) kwetu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana

**Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uoko-
lewe katika yeye."**

Yohana 3:16,17

Vifungu hivi vinatwambia kazi iliyokuwa ya Yesu na kazi ambayo haikuwa yake. Mungu alimtoa Yesu kwa watu wa ulimwengu kwa sababu aliwapenda watu wote. Ilikuwa kazi ya Yesu kuwaokoa watu katika dhambi zao. Hakuja kuhukumu ulimwengu, bali alikuja kuukomboa.

WAKATI WA KUFUNGA:

(Sema:) Ilikuwa ajabu sana kwa Yesu kuja ulimwenguni kutoka mbinguni kufanya kazi ambayo Mungu alimpangia. Yesu alijitoa yeye mwenyewe kufanya kazi ya Mungu katika njia ya Mungu.

(Uliza:) Je! unapenda kujitoa mwenyewe kwa Mungu kufanya jambo lo lote analokutaka kufanya? Dokeza kwamba kila kijana aombe maombi yake mwenyewe ya kujitoa kwa Mungu.

YULE ALIYE MKAMILIFU PEKEE

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo
4:1-11; Luka 4:1-13

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kujua kwamba Yesu pekee ndiye hana dhambi. Ingawa alikuwa na taabu na akakabili majaribu ambayo kila mtu hukabili, aliyashinda majaribu hayo na hakutenda dhambi.

Watoto ni werevu sana katika kutoa udhuru juu ya tabia zao, lakini mara kwa mara husumbuliwa na majaribu yanayowakabili. Ingawa wao hutoa udhuru, kwa kawaida hustaajabu pia ni kwa nini hutenda mambo wasiyotaka kufanya au jinsi wanavyoweza kushinda majaribu yatakapowajia tena.

Labda wanaweza kustaajabu pia juu ya Yesu. "Je! Yesu alikuwa na taabu katika kutenda haki kama mimi ninavyokabiliwa na taabu? Je! Yesu kama Mwana wa Mungu angeweza kumtotoi Mungu? Yesu alijua jambo la kufanya wakati ilipombidi kufanya uchaguo?" Katika somo hili unaweza kuwasaidia wanafunzi wako kujibu maswali haya.

Kwa kujitayarisha kamili, soma maandiko haya mengine zaidi: Yakobo 1:13-15; Marko 14:38; Yakobo 4:7; 1 Wakorintho 10:13; 2 Petro 2:9; Waebrania 4:15, 16; Yakobo 1:12.

Usisahau kusudi la somo hili wakati unapofundisha. Unayo nafasi ya kuwasaidia wanafunzi wako kuona kwa

hakika udhuru wanaotoa. Wasaidie kulinganisha hali yao ya kukubali majaribu na njia ambazo Yesu alionyesha matendo yake wakati Ibilisi alipomjaribu. Wanafunzi wako wanapaswa kujifunza kwamba Yesu anawafahamu na yuko tayari kuwasaidia na wanaweza kutumia njia aliyowapa ili waweze kushinda majaribu.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Ingawa Yesu alikuwa akimtii Mungu kabisa na kutoa maisha yake kwa kazi ya Mungu, bado alikuwa na taabu.
2. Yesu alikabili majaribu kama mtu ye yote anavyokabili.
3. Wakati Yesu alipojaribiwa, alijua kwamba angejaribiwa na alikuwa tayari kupinga majaribu hayo.
4. Yesu alijua Neno la Mungu na alilitumia katika kupinga majaribu yake.
5. Yesu alitaka kumtii Mungu ingawa ilikuwa vigumu.
6. Yesu atakusaidia kushinda majaribu katika njia kama ile aliyopinga majaribu yake.

KULIFUNDISHA SOMO:

Tuseme kwamba mama anakutuma sokoni kumnunulia kitu. Wakati unapoingia sokoni unakutana na rafiki anayekunong'onezea, "Na tuchukue kitu tunachotaka."

Unaangalia wakati rafiki huyo anapochukua kitu na kukificha mfukoni mwake. Halafu anakwambia kwamba atakuangalia mwuzaji wakati wewe pia unapochukua kitu na kukificha.

(Uliza:) Je! ungekuwa na mawazo gani juu ya jaribu hili? (Ungekuwa na mawazo kama haya: “Sijali”, “Kila mtu huiba,” au “Hakuna mtu atakayejua jambo nifanyalo,” “Nitafanya hivyo sasa peke yake,” au “Nataka kusema la, lakini nashindwa,” au “Rafiki yangu huyu atasema nini nikikataa kufanya kama anavyosema?”)

(Sema:) Kwa kawaida tunajua jambo jema linalotupasa kufanya lakini shida ni kwamba hatujui jinsi ya kupata nguvu ya kutenda jambo hilo jema. Je! tunaweza kumwendea Yesu wakati tunapojaribiwa? Atatusaidiaje?

(Sema:) Ingawa Yesu alimtii Mungu kabisa na kutoa maisha yake kwa kazi ya Mungu, bado alikuwa na taabu. Alijaribiwa kama kila mtu anavyojaribiwa.

Wakati Yesu alipokuwa na umri wa miaka thelathini aliondoka nyumbani kwao Nazareti akaenda katika Mto wa Yordani. Yohana alimbatiza huko. Baada ya ubatizo wake alikwenda peke yake nyikani kufikiria maneno ya Mungu na kazi ambayo Mungu alimtaka kufanya. Kazi yake ilikuwa kuwaonyesha watu jinsi Mungu alivyo. Alihitaji kuzungumza na Baba yake wa Mbinguni juu ya mipango yake. Alikwenda katika nyika ya Uyahudi, na katika nyika hilo Ibilisi alimpata kumjaribu.




Wakati Yesu alipokuwa akifikiria kazi yake kama Mwana wa Mungu, alifunga kula chakula. Alikaa peke yake nyikani siku arobaini mchana na usiku akifikiri na kuomba bila kula kitu cho chote. Kila siku aliendelea kusikia njaa.

Wakati Yesu alipotambua kwamba alikuwa na njaa sana, Ibilisi alimjia, akasema, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, unaweza kupata chakula kwa urahisi. Unaweza kuamuru kwamba mawe haya yawe mikate.”



Ibilisi alikuwa akimwambia Yesu, “Kuwa mchoyo.” Alikuwa akijaribu kumshawishi Yesu kutegemeza ufalme wa Mungu kwa vitu tu vya hapa duniani.


Yesu alijua kwamba alikuwa na uwezo wa kuamuru mawe kuwa mikate. Alikuwa amepewa uwezo huo kuwasaidia wengine wala siyo kuutumia katika njia ya choyo. Ingawa alikuwa mnyonge kwa sababu ya njaa, alikataa kuwa mchoyo. Alikumbuka kifungu kimoja cha Biblia alichojifunza wakati alipokuwa mdogo. Kifungu hicho kilisema ya kwamba kuna vitu fulani ambavyo ni vya umuhimu zaidi kuliko chakula. Kisha alimwambia Ibilisi aliyekuwa akimjaribu, "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa neno litokalo katika kinywa cha Mungu." (Mathayo 4:4) Yesu alimjibu Ibilisi kwa kutumia kifungu hicho kwa sababu hakutaka kutumia uwezo wa Mungu kwa kusudi la choyo.



Ibilisi alipoona kwamba Yesu alikataa kumtii kwa kuridhisha njaa yake, alimjaribu kwa njia nyingine ya

hila. Alimchukua Yesu mpaka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, "Yesu, najua kwamba unawataka Wayahudi wote kukuamini wewe kuwa ndiwe Mwana wa Mungu. Jitupe chini kutoka hapa juu. Na ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, Mungu hatakuacha kuumia. Atawatuma malaika zake kukuchukua mikononi mwao. Kisha kila mtu atakuamini."

Yesu alikumbuka tena kifungu ambacho ni lazima kukitii. Wakati huu Yesu alimwona Ibilisi, akamwambia, "Usimjaribu Bwana Mungu wako." (Mathayo 4:7) Yesu alikuwa akisema ya kwamba ilikuwa kosa kufanya jambo la kipumbavu na kumtumainia Mungu kukulinda usiumie. Ni kosa kutumia uwezo wa Mungu kuwalazimisha watu kuamini. Yesu alikataa kufanya kazi yake katika njia ambayo haikuwa ya haki.



Ibilisi alishindwa tena kwa sababu Yesu alijua Neno la Mungu na alilitumia kuyashinda majaribu yake. Lakini Ibilisi hakukata tamaa. Tena alijaribu kumshawishi Yesu kumtii. “Akampandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa ye yote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako.”


Kwa kweli Ibilisi alikuwa akimwambia Yesu, “Fanya kosa na kutumainia kupata mema kwa kosa hilo.”

Yesu aliwafikiria watu wote katika milki za ulimwengu. Alikuwa amekuja kuwaambia habari za ufalme wa mbinguni ambako angetawala na watu wangemwabudu Mungu. Pengine Yesu alifikiri, “Njia hii labda ingekuwa njia rahisi sana ya kuwa mfalme wa watu wote. Kama ningekuwa Mfalme ningewafanya watu wote kumwabudu Mungu.”

Lakini Yesu alijua kwamba ingekuwa dhambi kumwabudu Ibilisi. Alikataa kutenda dhambi na kutumainia kwamba mema yangetoka katika dhambi hilo. Yesu alimjibu Ibilisi bila kusita kwa kutumia Neno la Mungu lisemalo, “Imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.” (Mathayo 4:10)

Ibilisi alikuwa amekwisha kufanya kila jambo aliloweza, lakini hakupata njia ya kumlazimisha Yesu kutenda dhambi. Yesu, Mwana wa Mungu, aliye mkamilifu pekee, hakukubali majaribu

ya Ibilisi kwa sababu alijua Neno la Mungu na alilitumia kuyashinda majaribu hayo.



*Msujudie Bwana
Mungu wako.*

Tumekwisha kuona jinsi watu wanakuwa na mawazo tofauti wakati wanapojaribiwa. Na tufikirie hadithi hii ya Biblia na kuona kama tunaweza kukumbuka njia ambazo Yesu alionyesha matendo yake wakati alipojaribiwa.

1. Alitazamia majaribu kuja.
2. Alijua Neno la Mungu na alilitumia kushinda majaribu.
3. Alitaka kumtii Mungu.

(Sema:) Baadhi yenu wanaweza kufikiri kwamba; kwa vile Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, hakuwa na ugumu wo wote wa kushinda majaribu. Lakini kuna neno katika kifungu cha kukumbuka linalotwambia kwamba

Yesu alijaribiwa kweli. (Huu ndio wakati mzuri wa kufundisha kifungu cha kukumbuka Waebrania 1:18).

(Uliza:) Je, ni neno lipi linalotwambia kwamba Yesu alijaribiwa kweli? (Aliteswa.)

Ndiyo, Aliteswa. (Uliza:) Je! neno hili maana yake ni nini? (Maana yake ni kwamba alishinda majaribu mpaka mwisho ingawa ilikuwa vigumu kufanya hivyo.)

Hatuhitaji kuona aibu wakati tunapojaribiwa kwa sababu kujaribiwa siyo dhambi. Kwa sababu Yesu aliteswa alipojaribiwa, anafahamu taabu ambayo Ibilisi hutupa wakati mwingine. Yesu anafahamu na hutusaidia mara moja wakati tunapomwendea kutupa msaada wa kushinda mapendekezo ya Ibilisi.

(Uliza:) Yesu hutusaidia kushinda majaribu? (Rudia mambo yale matatu ambayo yamekwisha kutajwa.) 1. Yesu alitazamia majaribu kuja. 2. Alijua Neno la Mungu na alilitumia kushinda majaribu. 3. Alitaka kumtii Mungu ingawa ilikuwa vigumu.

(Sema:) Kwa sababu Yesu yu hai na yupo pamoja nawe kama u Mkristo, atakusaidia kushinda majaribu katika njia ile kama yake aliyoshinda majaribu.

KAZI YA KUFANYA:

Tafuta majibu ya maswali haya juu ya majaribu katika Neno la Mungu (Biblia).

Je! jaribu hutoka wapi?

Soma Yakobo 1:13-15 kisha uchore mviringo kwa herufi "K" iliyo kando ya

sentensi ya kweli. Chora mviringo kwa herufi "M" iliyo kando ya sentensi ambayo si kweli.

(K) M Mungu hanijaribu mimi.

(K) M Mimi hujaribiwa ninapofuata tamaa zangu.

(K) M Tokeo la kukubali jaribu ni dhambi.

K (M) Tokeo la dhambi ni uradhi.

Je! yanipasa kuwa na mawazo gani juu ya jaribu?

Soma Marko 14:38 na Yakobo 4:7 halafu kata maneno yote yaliyo katika alama hii () ambayo si kweli.

Yesu aniambia (~~kufanya kazi~~) (kukeshwa) nikiomba ili nisije nikaingia majaribuni.

Ingawa (~~mwili~~) (roho) yangu iko tayari kushinda majaribu, (~~mwili~~) (~~roho yangu~~) wangu u dhaifu. Yanipasa kujitoa mimi mwenyewe kwa (~~jaribu~~) (Mungu).

(~~Nikikubali~~) (Nikimkataa) Ibilisi, atakimbia kutoka kwangu.

Je! yanipasa kukubali wakati ninapojaribiwa?

Soma 1 Wakorintho 10:13 na upige mstari chini ya sentensi unayofikiri kuwa inakusaidia kujua maana ya kifungu hiki.

Kwa vile naona ya kwamba majaribu yangu ni magumu zaidi kuliko ya wengine, najua sitakuwa na nguvu za kuyashinda.

Mungu atanipa njia daima ili nisiweze kuyakubali majaribu.

Je! ni nani atakayenisaidia kupata njia ya kushinda majaribu wakati ninapojaribiwa?

Soma 2 Petro 2:9 na uandike katika mstari huo jina la yule atakayekusaidia wakati unapojaribiwa. Bwana

Je! yanipasa kufanya nini wakati ninapojaribiwa?

Soma Waebrania 4:15,16 na kuandika namba kando ya sentensi zifuatazo kama inavyofaa. (Andika namba 1 kando ya sentensi unayofikiria kuwa ni ya kwanza na kuandika namba 2 kando ya sentensi ya pili, n.k.)

2 Yesu alijaribiwa sawa-sawa nami, lakini haku-fanya dhambi.

3 Naweza kumwendea Yesu na kumtumainia kunipa msaada wakati wa mahitaji.

1 Yesu afahamu udhaifu wetu.

Je! ni nani anayejua na kujali kwamba ninashinda majaribu yangu?

Soma Yakobo 1:12 na kujibu swali hilo juu katika mstari ufuatao.

Mungu anajua na kujali wakati ninapopinga majaribu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.”

Waebrania 2:18

Kuna dokezo kuhusu mafundisho ya matumizi ya kifungu maalum pamoja na wanafunzi wako katika sehemu ya “Kulifundisha Somo.”

WAKATI WA KUFUNGA:

Zungumza na wanafunzi wako kuhusu njia ambazo wao hujaribiwa mara kwa mara kama kusema uwongo, kuiba, na kutotii wazazi, kufanya kazi yao isiyo nzuri, kusahau kuomba, au kupenda kitu au kumpenda mtu mwingine zaidi kuliko Mungu.

Zungumza nao jinsi wanavyoweza kutumia neno la Mungu kushinda majaribu kama wakikabiliwa na majaribu yafuatayo:

Kusema uwongo - Wakolosai 3:9

Kuiba - Kutoka 20:16

Kutowatii wazazi - Waefeso 6:1

Kutofanya kazi kwa njia nzuri - Wakolosai 3:23

Kusahau kuomba - Luka 18:1

Kupenda kitu au kumpenda mtu mwingine zaidi kuliko kumpenda Mungu - Mathayo 10:37; 22:37.

(Labda utapenda kufunga somo lako kwa maombi, mkiomba pamoja kuhusu mahitaji ya wanafunzi wako na kushukuru kwa njia ambayo Mungu ametoa kwa kushinda majaribu.)

MWALIMU ANAYETOKA KWA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 1:35-51; Mathayo 4:18-25; 10:1-31; Luka 6:12-16

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Wanafunzi wako wanahitaji kujifunza ya kwamba kusikia na kutenda neno la Mungu ni mambo mawili yanayoshikana pamoja na yote ni ya muhimu sana. Tokeo la kujifunza neno ni kutenda, lakini kitendo cha haki kinapaswa kutegemezwa kwa ukweli halisi wa Neno la Mungu. Ufahamu huu hutoka kwa Neno la Mungu na kwa mwalimu hasili ambaye ni Yesu Kristo.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kujua kwamba Yesu alitumwa na Mungu kuwa mwokozi wetu na mwalimu wetu ili tungeweza kujifunza kwa mambo aliyoyasema na kuyafanya. Waongoze wanafunzi wako kuwa na nia ya kuonyesha mambo ambayo wamekwisha kujifunza kwa Yesu kwa kutenda na kusikia Neno la Mungu.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu alikuwa mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu kutufundisha kwa mfano mambo ambayo Mungu alitaka kujifunze.
2. Yesu aliwaita wanafunzi wake na kuwafundisha. Wanafunzi walijifunza kwa mfano wake na kwa kufanya mambo aliyokwisha kuwafundisha.

3. Mungu hutusaidia kujifunza katika njia nyingi. Mojawapo ya sababu ya Yesu kuja ulimwenguni ni kwamba angetufundisha njia ya Mungu na kutudhihirishia Mungu.

4. Tunaonyesha kwamba tumekwisha kujifunza kweli Neno la Mungu wakati tunapokuwa “watendaji” wa neno wala sio “wasikilizaji” tu.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Uliza:) Je! unajua jinsi mtu anavyojifunza kuendesha motakaa? Kwanza, hupata kitabu cha maongozi ya kuendesha motakaa kutoka kwa afisi wa kutoa cheti cha kuendesha motakaa na kujifunza maongozi yaliyomo ndani ili apate kujua sheria za kuendesha motakaa. Kisha humtafuta mwalimu wa kumwambia jambo la kufanya na kumwangukia mwalimu huyo jinsi anavyofanya jambo hilo. Halafu hujaribu kuendesha motakaa yeye mwenyewe.

(Uliza:) Mtu atajua ya kwamba amekwisha kujua kuendesha motakaa? (Atajua wakati anapoweza kuendesha motakaa yeye mwenyewe bila msaada wote. Uliza:) Serikali itajua ya kwamba anaweza kuendesha motakaa? (Kwa kumpa mtihani.) Labda anaweza kupewa mtihani wa kuandika ili kuonyesha kweli kwamba anajua sheria za kuendesha. Pia atapewa mtihani wa kuendesha barabarani kuonyesha kwamba anaweza kuendesha vizuri na kufuata sheria za barabara. Anapopita mtihani hiyo, anapewa cheti.

Maisha yetu yamefanana na motakaa. Maisha yetu pia ni lazima kuendeshwa vizuri kulingana na sheria za usalama na ushindi. Mungu anatutaka sisi sana kujua jinsi ya kuishi maisha mema.

Mungu hatuachi katika hali ya kuchanganyikiwa kuhusu njia yake kwa furaha. Ingawa hatuwezi kujua kila kitu juu ya Mungu, tunaweza kuendelea kutambua mambo mapya juu ya Mungu, jinsi alivyo, jinsi anavyofanana, na maongozi ambayo amekwisha tupatia ili kumpendeza na kukaa kwa furaha.

Yohana alisimama pamoja na wanafunzi wake wawili wakamtazama Yesu akitembea kuwaelekea wao. Yohana alisema, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu." (Yohana 1:36) Mara wanafunzi hawa walianza kumfuata Yesu. Walifurahi kupokea mwaliko wa Yesu wa kukaa pamoja naye siku ile.

Mmojawapo wa wanafunzi hao alikuwa Andrea. Alikuwa na furaha mno hata akaenda kumtafuta Simoni Petro nduguye. Alipompata, alimwambia, "Tumemwona Masihi." Alimleta Simoni Petro kwa Yesu.



(Uliza:) Mungu hutufundishaje, na tunajua je ya kwamba tumekwisha kujifunza?

Somo hili linatwambia jinsi Yesu alivyowaita wafuasi wake na kuwafundisha wakati walipokuwa hapa ulimwenguni miaka mingi sana iliyopita.

Kesho yake Yesu aliamua kwenda Galilaya. Alipokuwa njiani kwenda huko, alimwona Filipo. Alimwambia Filipo, "Nifuate." Filipo alifanya kama alivyosema. Kisha Filipo naye alimwona Nathanieli, akamwambia habari za Masihi. Wakati Yesu alipomwona Nathanieli alisema ya kwamba

alikuwa mtu mwaminifu. Andrea, Yohana, Petro, Filipo, na Nathanieli ndio waliokuwa marafiki na wanafunzi wa kwanza wa Yesu.

(Uliza:) Je! wanafunzi hawa kwanza walijifunza nini juu ya Yesu? (Walijifunza kwamba alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu.) Je! Andrea alipotambua hivyo, alifanya nini? (Alikwenda kumtafuta Simoni Petro na kumleta kwa Yesu.) Je! Filipo alipotambua hivyo, alifanya nini? (Alimleta Nathanieli. Sema:) Tunaposhawishika hasa ya kwamba kitu fulani ni kweli, tunakuwa na moyo wa kufanya jambo fulani juu yake.

Wakati mwingine baadaye Yesu alikwenda kukaa katika mji wa Kapernaumu katika Ziwa la Galilaya. Siku moja, wakati alipokuwa akitembea kando ya Ziwa hilo, aliwaona wale marafiki zake wawili, Andrea na Petro. Walikuwa wakivua samaki. Walivua samaki kwa kutumia wavu mpana. Bila shaka Yesu aliwatazama wale marafiki zake kwa muda. Kisha aliwaambia kwamba angewafundisha jinsi ya kuvua vitu vingine tofauti na samaki. Alisema, "Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." (Mathayo 4:19) Walimfuata. Wote watatu walitembea kando ya Ziwa. Waliwaona ndugu wengine wawili; Yakobo wa Zebedayo na Yohana nduguye, ambao walikuwamo ndani ya mashua pamoja na Zebedayo baba yao. Wote watatu walikuwa wakitengeneza nyavu zao. Yesu aliwaita Yakobo na Yohana kuacha kazi yao na kumfuata. Mara waliacha mashua yao na baba yao, wakamfuata.

(Uliza:) Je! Andrea, Petro, Yakobo, na Yohana walijifunza nini? (Walijifunza kwamba Yesu angewapa maisha ya furaha kama wangepasaidia watu kumjua Yesu kwa kuwafundisha na kuhubiri.) Uliza: Je! walipojifunza hayo walifanya nini? (Waliacha kila kitu na kufanya kama Yesu alivyowaambia.) Sema: Tunaposhawishika hasa ya kwamba kitu fulani ni kweli, tunakuwa na moyo wa kufanya jambo fulani juu yake.

Mkutano wa watu wengi walimfuata Yesu. Wote walistaajabia mambo ya kushangaza ambayo Yesu alikuwa akifanya. Yesu alikuwa akiponya viwete na vipofu na wagonjwa. Watu wengine walistaajabu sana hata wakamfuata Yesu kila mahali alipokwenda, wakawa wanafunzi wake. Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni. Mojawapo ya mambo mengi ambayo Yesu alifanya lilikuwa kuwafundisha watu. Aliwafundisha watu juu ya ufalme wa Mungu. Aliwafundisha maana ya kuwa wanafunzi wake.

Kulikuwa na watu wengi sana waliohitaji kujua ukweli na nguvu za Mungu ya kwamba Yesu alihitaji msaada. Siku moja jioni, Yesu alipanda mlimani akakesha usiku kucha katika maombi. Alimwomba Mungu kumsaidia kuwachagua watu waliofaa kwa kazi maalum ya kuendelea kutimiza kazi yake. "Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake; akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita mitume." (Luka 6:13)

(Uliza:) Je! wanafunzi hao walijifunza nini juu ya kufanya

uchaguo? (Walijifunza kwamba wakati walipokuwa na uchaguo maalum wa kufanya, iliwapasa kumwomba Mungu msaada.) Je! walijifunza nini juu ya kuitenda kazi ya Mungu? (Walijifunza kwamba mtu akitaka kutimiza kazi ya Mungu ni lazima kusikia neno lake na kulitenda, wala siyo kusikia tu. Pia mtu atendaye kazi ya Mungu ni yule aliye na nia ya kuitenda kazi hiyo. Sema:) Tunaposhawishika hasa kwamba kitu fulani ni kweli tunakuwa na moyo wa kufanya jambo fulani juu yake.

Ilikuwa wakati mwingine baada ya Yesu kuwachagua mitume wake. Mitume hawa walikwisha kukaa naye na kumsikia akifundisha na kumwona akifanya miujiza. Sasa ulikuwa wakati kwao kutumia mambo waliyojifunza katika kutenda. Kwa hiyo Yesu aliwaeleza kwa uangalifu kazi ambayo wangepanya na jinsi ambavyo wangepanya kazi hiyo.



Kazi yao ilikuwa kutembea wawili wawili kwenda katika miji yote, kufanya miujiza ya kuponya kama Yesu alivyofanya, na kuwafundisha watu juu ya Masihi. Hawakupaswa kuwa na wasiwasi kwamba wangepuka nini, kuvaa nini, kwamba watu waliwape-nda, au la. Hawakupaswa kuwa na wasiwasi kama wangeshikwa na kuletwa mbele ya maliwali, wafalme, au mabaraza. Roho wa Mungu angewafundisha mambo ya kusema. Hawakupaswa kumwogopa mtu ye yote kwa sababu watu wangeweza kuua miili yao tu lakini siyo roho zao. Mungu alijua mateso yao kama vile anavyojua wakati shomoro (ndege) anapoanguka chini kutoka angani. Wao walikuwa wa thamani nyingi kwa Mungu kuliko mashomoro. Mungu angewasaidia kukamilisha kazi yao.

(Uliza:) Mitume walikuwaje bado wakijifunza wakati walipotumwa wawili wawili kwa kazi ya Bwana? (Walikuwa wakijifunza kwa kutenda.) Walijifunza nini kwa kutenda? (Walijifunza kutumia uwezo ambao Yesu aliwapa kuwaeleza wengine habari za Yesu na kuwa mashujaa na kutoogopa.) Tunaweza kuzungumza juu ya mambo haya lakini tunaonyesha kwamba tumekwisha kujifunza mambo haya kwa kuyajaribu katika matendo yetu. Tunapoyajaribu ndipo tunapojifunza mengi zaidi. (Sema:) Tunaposhawishika hasa kwamba kitu fulani ni kweli, tunakuwa na moyo wa kutenda jambo fulani juu yake.

Mbeleni tulisema ya kwamba Mungu anatutaka sisi kujua jinsi ya kuishi

maisha mema kama dereva mwema anavyoendesha motakaa. Mungu alitupa mwalimu bora wa kutuhakikishia kwamba tuna maongozi mema. (Uliza:) Je! mwalimu huyo ni nani?

Yesu ndiye aliyekuja kutueleza na kutuonyesha kila kitu ambacho Mungu alitutaka kujua. Yesu ndiye ufunuo wa Mungu, ndiye yule anayetufundisha ukweli wa Mungu.

(Uliza:) Je! ni njia ipi nyingine nzuri ambayo Mungu hutufundisha? Ndiyo, alimtuma Yesu kuwa mwalimu wetu.

KAZI YA KUFANYA:

Hapo chini kuna maandiko manne ya Biblia. Soma kila mojawapo, halafu piga mstari kutoka kwa kila andiko hadi maneno yaliyo upande wa kulia ambayo yanapatikana katika andiko hilo. Hizi ni baadhi ya njia ambazo Mungu hutumia kutufundisha.

Mithali 3:5	—	Mtumaini Bwana
Yakobo 1:5		Mwana wa Mungu
Yohana 14:26		Roho Mtakatifu
Waebrania 1:1,2		Maombi (kumwuliza Mungu)

Soma Luka 6:12-16. Katika vifungu hivi utapata majina ya wanafunzi kumi na wawili wa Yesu. Jaza nafasi zilizoachwa ili kukamilisha majina hayo.

Petro	<u>Mathayo</u>
<u>Andrea</u>	<u>Tomaso</u>
<u>Yakobo</u>	<u>Yakobo</u> (wa Alfayo)
<u>Yohana</u>	<u>Simoni</u>

Filipo	<u>Yuda</u> (wa Yakobo)
Bartolomayo	<u>Yuda</u> Iskariote

Katika somo la wanafunzi kuna picha ya Yesu akiwafundisha baadhi ya wanafunzi wake. Wape wanafunzi nafasi ya kupaka picha hiyo rangi kwa kutumia kalamu za rangi kama unazo. Kama huna kalamu za rangi, tumia kaa.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidaganya nafsi zenu."

Yakobo 1:22

WAKATI WA KUFUNGA:

(Uliza:) Je! unakumbuka kutokana na hadithi ya Biblia jinsi Yesu alivyowasaidia mitume kujifunza? (Wasaidie wanafunzi wako kukumbuka ya kwamba mitume wale walijifunza kwa 1) *kusikiliza* Neno la Mungu, kwa kumsikiliza Mwana wa Mungu, kwa kumsikiliza Roho Mtakatifu, na kwa kusikilizana wao kwa wao wakati walipotumwa wawili wawili; 2) kwa *kutazama* mambo ambayo Yesu alifanya kuwa mfano kwao, kama vile Yesu alivyoomba; (3) kwa *kufanya* kazi wao wenyewe.

(Uliza:) Je! tunajua kwa jinsi gani ya kwamba tumekwisha kujifunza jambo? (Wakati tunapofanya jambo hilo vyema.) Kifungu chetu cha kukumbuka kinaeleza wazi juu ya jambo hili.

(Sema:) Fikiria tena mambo tuliyojifunza kuhusu Yesu ni nani. Tumejifunza kwamba yeye ni Masihi na yule hutufahamu, ni Mwana wa Mungu aliye na kazi maalum, hana dhambi, na

ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu. Na tufikirie mambo yanayotupasa kufanya kwa sababu tumekwisha kujifunza mambo haya.

Inatupasa kumsujudia Mwokozi. Inatupasa kuwa katika hali ya kufarijiwa na kuwafariji wengine. Inatupasa kujitoa wenyewe kwa Mungu na kuitafuta kazi ambayo Mungu anataka tufanye. Inatupasa kushinda majaribu. Inatupasa kusikia na kutenda

neno la Mungu. Fikiria mambo haya na kukata shauri juu ya mambo hasa utakayofanya ili kuwa mtendaji wa neno wala si msikilizaji tu.

(Uliza:) Je! ni njia ipi ambayo Mungu hutufundisha na ambayo tunaweza kuitumia wakati wa kufunga somo hili letu? (Ndiyo, ni maombi. Waambie wanafunzi kuomba, na kila mmoja aombe msaada wa kufanya mambo ambayo Mungu anamtaka kufanya.)

WAKATI TUNAPOPINGA MATENDO MABAYA

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 2:13-25

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Mtu hawezi kufundisha jambo asilojua. Ni muhimu kwako kujifunza somo hili mara kadha mpaka unapolielewa kabisa kabla ya kuweza kufundisha kwa njia inayofaa.

Siyo kujifunza tu kabla ya wakati wa kufundisha, bali unahitaji pia kuomba ili Mungu akusaidie kufundisha ukweli wake wa kiroho katika njia zitakazowasaidia wanafunzi wako kufahamu.

Kama wanafunzi wako wanavyofahamu, kuna mambo mengi mabaya yanayofanywa ambayo wao huona. Unahitaji kuwasaidia kufahamu jambo wanaloweza kufanya kuhusu mambo hayo mabaya wanayoyaona yakifanywa. Itakuwa vema kuwaambia juhudi kamili ya Kikristo ya kusahihisha matendo mabaya.

Kwa maana Yesu ni mfano kamili, utataka kuonyesha mambo aliyofanya wakati alipowaona watu wakitenda mambo mabaya. Hakupenda kutazama matendo mabaya. Lakini zaidi ya hayo, alifanya jambo fulani kukomesha matendo hayo mabaya.

Kwa maandiko mengine zaidi, itakupasa kusoma Isaya 59:1,2 inayonyesha kwamba Mungu ni Mtakatifu, na kwamba dhambi hutenga watu na Mungu. Utaona katika Yohana 3:16,17 ya kwamba Mungu anatupenda na

alimtuma Mwanawe kutuokoa. Yohana 1:12 inatwambia kwamba wote wanaomwamini Yesu aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu. Katika Tito 3:8 tunaambiwa kwamba Wakristo wanapaswa kutenda matendo mema. Na katika Wagalatia 6:1 Wakristo wanashauriwa kusaidiana ili wapate kutenda haki.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kufahamu kwamba inatupasa kutenda kazi nzuri na kupinga matendo mabaya.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu, ambaye ni mwenye haki, alionyesha kwamba Mungu anachukia uovu.
2. Inatupasa kufunua matendo mabaya kwa utii wetu kwa Kristo.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Uliza:) Je! Wakristo wanapaswa kupinga? Ikiwa wanapaswa kupinga, basi wanapaswa kupinga nini?

(Sema:) Tuna mfano katika maandiko ya somo hili unaotonyesha mambo ambayo Yesu alipinga.

Tunaposoma historia kuhusu desturi katika siku za Yesu, tunajifunza ya kwamba kulingana na sheria ilikuwa muhimu kwa matoleo ya hekalu kutolewa kwa nusu Shekeli. Jambo hili liliwalazimu watu waliotoka Uajemi, Shamu, Misri, Uyunani, au Rumi kubadilisha pesa zao katika nusu Shekeli ya hekalu. Walitozwa pesa kwa

utumishi huu, na wavunja pesa walitajirika sana.

Ilikuwa wakati wa mwezi wa Aprili na wakati huu ulikuwa maalum sana mwakani. Ulikuwa wakati wa Sikukuu ya Pasaka. Katika mwezi uliotangulia sikukuu hii, watu walitengeneza madaraja na barabara zilizoongoza kuingia mjini Yerusalemu. Hata walipaka makaburi chokaa.

Wakati Sikukuu ya Pasaka ilipokaribia, wavunja pesa walihamisha shughuli zao hadi hekaluni katika chumba cha watu wa Mataifa ambako kulikuwa na vitu vingi sana vya kununuliwa na waabudu kwa sikukuu yao ya kidini. Kwa sababu ilikuwa ni lazima kutumia pesa za hekalu kwa kila kitu walichokinunua, daima palikuwapo mabishano mengi na mashindano na piganio la bei.


Palikuwapo pia biashara nyingine zilizokuwa zikiendeshwa mahali pale kwa sababu sheria ya kidini iliamuru kutolewa sadaka ya kondoo na maksai (ng'ombe dume). Wanyama hawa walichinjwa kuchukua mahali pa hatia ya watu na kulipa deni la dhambi zao. Wanyama hawa pia waliongeza kelele kuwa nyingi sana hekaluni.

Wavunja pesa walitumia chumba kile hekaluni ambacho watu wa mataifa kulingana na desturi walikuja kuabudia. Jambo baya sana ni kwamba soko hili liliendeshwa na watu wachoyo waliowaibia watu pesa zao kwa kuwatoza malipo ya juu. Hakuna mtu aliyependa jambo hili, watu na viongozi wa dini hawakulipenda, lakini hakuna mtu aliyethubutu kuhatarisha maisha yake kwa kumpinga mkuu wa sheria

ambaye alikuwa kuhani mkuu.

Kisha Yesu alikuja!

Yesu alitazama shughuli zile zote zilizokuwa zikiendeshwa mle ndani ya hekalu. Alikwenda katika sehemu palipowekwa wanyama wa kutolewa sadaka. Alifanya kikoto cha kamba. Kwa kikoto hicho, aliwatoa ng'ombe na kondoo wote katika hekalu.



Yesu alipokwisha kuwatoa wanyama hao nje, alikwenda kwa meza ya wavunja pesa. Alipozifikia meza hizo, alianza kuzipindua moja moja na kumwaga pesa za wenye kuvunja pesa.



Kisha aliwaamuru watu waliouza njiwa, "Yaondoeni haya; msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara." (Yohana 2:16) Watu walijua kwamba shughuli hizi hazikupasa kuendeshwa hekaluni, na walijua kwamba wafanya biashara hao walikuwa wakiwaibia.

Viongozi wa dini walikuja, wakamwuliza Yesu, "Una haki gani ya kuwatoa watu wale nje ya hekalu? Ikiwa una uwezo wa Mungu, tuonyeshe mwujiza wa kuuthibitisha."

Yesu aliwapa jibu ambalo hawakufahamu. Badala ya kufanya mwujiza mkuu kama walivyomtumainia kufanya, aliwaambia, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." (Yohana 2:19)

Viongozi wa Wayahudi walimkumbusha ya kwamba ujenzi wa hekalu hili ulichukua muda wa miaka arobaini na sita na ulikuwa bado haujamalizika. Yesu alikuwa na maana gani kwa maneno hayo?

Baadaye tu watu walianza kufahamu maneno yale ambayo Yesu aliyasema hekaluni. Baada ya mwili wake "kuharibiwa" katika mauti ya kusuliwa, na katika muda wa siku tatu ambapo Yesu alipofufuka, wanafunzi wake walitambua kwamba Yesu alinena habari za hekalu la mwili wake, wala si habari za hekalu la mawe.

(Uliza:) Je! Yesu aliwaza nini moyoni alipoona shughuli zile zilizokuwa zikiendeshwa hekaluni? Je! ilikuwa haki kwake kukasirika?

(Sema:) Jaribu kukumbuka wakati (wa hivi karibu) ambapo ulikasirika sana na sababu iliyokufanya kukasirika hivyo. Utaona kwamba kwa kawaida hasira zetu hutokana na mambo tunayofikiria kuwa si haki kwetu, hasa wakati madhumuni yetu yanapozuliwa. Yesu alikasirika kwa sababu ya mambo ambayo hayakuwa haki. Tunasema hasira yake kuwa ni hasira ya "haki," hasira kwa ajili ya kutaka haki itendwe, au kwa kutaka sababu takatifu idumishwe.

KAZI YA KUFANYA:


Yesu ndiye mfano wetu wa kweli. Jibu maswali haya yafuatayo kuhusu mambo ambayo Yesu alifanya katika somo hili letu.

Je! Yesu alipinga nini? Matendo mabaya katika nyumba ya Mungu.

Yesu alikuwa akipinga kwa jinsi gani? Aliwatoa wavunja pesa.

Kwa nini Yesu alikuwa akipinga? Ili watu wataweza kuabudu na salama.

Tunapoona matendo mabaya tunaweza kufuata mojawapo ya njia nne zinazoonyesha (katika ukurasa unaofuata huu). Chora mishale kutoka kwa picha ya mtu aliyechorwa mpaka kwa maneno yanayotwambia mambo ambayo Yesu anātutaka sisi kufanya wakati tunapoona matendo mabaya.



Kwa kusoma maandiko, tunaweza kutambua jinsi Mungu anavyotaka tuonyeshe tabia zetu wakati watu wanapoendelea kutenda mabaya. Tazama kila andiko la Biblia na kuona kama maneno hayo yanatoa maana uliyopata katika kifungu cha Biblia. Chora mviringo kwa "kidole kinachoeleza juu" kama jibu lako ni NDIYO. Chora mviringo kwa kidole kinachoelekeza chini" kama jibu lako ni HAPANA.



Soma Zaburi 145:17

Bwana ni mwenye haki katika mambo anayoyatenda, lakini huwezi kuyategemea mambo hayo.

NDIYO

HAPANA




Soma Isaya 59:1,2

Mungu yuko karibu sana na huwasikia na kuwasaidia wale wanaotenda maovu kama anavyowafanyia wale wanaotenda mema.

NDIYO

HAPANA



Soma Zaburi 5:4-6

Mungu hapendezwi na matendo maovu ambayo watu hutenda.



Soma Waebrania 1:8,9

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, huchukia maovu kama Mungu anavyochukia.

NDIYO

HAPANA



Soma 3 Yohana 11

Tunaweza kupatana na watu wanaotenda mabaya ikiwa hatuna shida nao.

NDIYO

HAPANA



Soma 2 Wakorintho 5:10

Siku moja Yesu atahukumu matendo yetu kama ni mema au mabaya.

NDIYO

HAPANA



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali myakemee.”

Waefeso 5:11

Mara nyingi ni vigumu sana kwa mtu mmoja kushindana na kundi la watu wengi. Ikiwa watu wote wanatenda mambo mabaya, sisi hujaribiwa kujiunga pamoja nao kutenda mabaya hayo badala ya kuwa peke yetu na kutoshiriki katika mabaya hayo. Yesu anatuonya ya kwamba tusijiunge na watu hao katika kutenda mabaya bali tuwakemee.

Pengine itakuwa ya kutosha kama hutashiriki nao tu. Na utawaonyesha kwa matendo yako kwamba wanatenda

mambo mabaya na kwamba hutaki kushiriki katika matendo hayo mabaya.

Lakini wakati mwingine baadaye itakuwa muhimu kuchukua hatua ya kupinga matendo yao mabaya kama Yesu alivyofanya katika somo hili.

Lakini katika njia yo yote, mioyo yetu inapaswa kuwa haki mbele za Mungu.

WAKATI WA KUFUNGA:

Katika kufunga somo hili utataka kukaza tena umuhimu wa kupinga matendo mabaya.

Omba ya kwamba Mungu atatusaidia kuona dhambi iliyo katika maisha yetu sisi wenyewe na pia kutusaidia kuwaonyesha wengine njia ya haki kwa maneno na matendo yetu ya haki.

WAKATI TUNAPOHITAJI MSAMAHA

MASOMO YA BIBLIA: Marko 2:1-12; Luka 5:17-26; Mathayo 9:1-8

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Kila mtu amekuwa na hatia. Hatia huwafanya watu kuwa na taabu kubwa. Hatia ni kujua kwamba tumetenda dhambi. Vijana na wazee wanajua hasa mawazo ya hatia.

Hadithi ya Biblia katika somo hili inaonyesha jinsi Yesu alivyoonyesha uwezo wa Mungu wa kuondoa taabu. Mtu anaweza kuwa na hatia, lakini hahitaji kuendelea kuubeba mzigo wa hatia hiyo yake. Yesu alikuja ulimwenguni, akafa msalabani ili tuweze kupokea msamaha wa dhambi na kuwa huru bila hatia.

Je! wewe ukiwa kama mwalimu unawaza moyoni mwako kuwa una hatia juu ya kitu cho chote? Ikiwa unawaza hivyo, mwombe Mungu kukusamehe. Katika somo hili lote jaribu kuwaonyesha wanafunzi ya kwamba wanaweza kutubu dhambi zao kwa Mungu na kupokea msamaha pia.

Kwa mafunzo zaidi ya Biblia juu ya Mungu anayesamehe dhambi, itakupasa kusoma 2 Mambo ya Nyakati 7:14, Zaburi 79:9, 1 Yohana 1:9, na Warumi 4:7.

Wanafunzi watafahamu vyema msamaha wa Mungu kama utawaambia jinsi ulivyopata kuokolewa. Labda baadhi ya wanafunzi wako ni Wakristo, na labda watapenda kusimulia juu ya wokovu wao.

Tunaimarika sana imani yetu wakati tunaposikia ushuhuda wa Mkristo mwingine.

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Mungu atatusamehe dhambi kama tukimwamini.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu, ambaye ni Mtakatifu, alionyesha tamaa na uwezo wa Mungu wa kusamehe dhambi.
2. Inampasa kila mtu kuamini uwezo wa Mungu wa kusamehe dhambi ili aweze kuupokea.
3. Mtu yule mwenye kupooza alihitaji kuponywa kiroho zaidi kuliko kuponywa kimwili.
4. Kama tunavyoendelea kutenda dhambi mara kwa mara ndiyo tunavyohitaji msamaha wa Mungu.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Uliza:) Tunapotenda dhambi, kama kusema uwongo, kuchukua kitu kisicho chetu, au kutowatii wazazi wetu, tunakuwa na mawazo gani?

(Sema:) Tunapofanya dhambi, tunawaza miyoni mwetu kuwa na hatia na kuogopa. Tunataka kujificha. Inakuwa vigumu sana kwetu kuonana uso kwa uso na mtu ambaye tumemkosea. Tunaona kuwa ni vizuri kutengana na mtu tuliyemkosea kuliko kukaa karibu naye. Dhambi hututenga na wengine. Dhambi hututenga na Mungu pia, kwa hivyo tunajaribu kumwepuka. Tunajiona kuwa wachoyo

na wenye huzuni na hatutaki kumsogea karibu.

Mungu hataki tutengwe naye kwa sababu ya dhambi. Ana uwezo wa kutusamehe dhambi zetu na anataka kufanya hivyo. Yanayotupasa kufanya ni kutubu dhambi zetu na kumwomba kwa juhudi kutupa msamaha wake kamili. Hadithi yetu ya Biblia inatuonyesha jinsi Yesu alivyoonyesha uwezo wa Mungu juu ya shida za kiroho na za kimwili. Baada ya Yesu kurudi Kapernaumu alihubiri ndani ya nyumba iliyokuwa imejaa watu wengi. Hapakuwa na nafasi kwa watu waliokuja nyuma kuketi ingawa walitaka sana kumwona Yesu na kumsikia. Lakini kulikuwa na watu wengine nje ambao waliwaza kwamba ilikuwa lazima wao kumwona Yesu. Kama haingalikuwapo huo uwezekano wa kupita mlangoni, basi wangelifikiria njia nyingine. Walikuwa na imani kwamba kama wangeingia nyumbani mle, Yesu angewatimizia haja yao. Walikata shauri kupanda juu ya dari ya nyumba ile, wakatoboa tundu ya kutosha kumpitishia mtu.



Watu wale wanne waliotoboa tundu darini walikuwa wakimbeba rafiki yao mwenye kupooza. Rafiki huyo alihitaji msaada ambao Yesu pekee ndiye angeweza kumpa. Hakuweza kujisaidia mwenyewe. Marafiki zake walimbeba mpaka juu ya dari. Kisha walitelemsha godoro alilolalia mpaka mbele ya Yesu.

Mtu yule mwenye kupooza sasa alikuwa mbele ya Yesu. Yesu alipoinua macho yake na kutazama tundu lile darini, aliona nyuso za marafiki wale wanne waliokuwa na imani. Aliona mengi kwao. Aliona mioyo yao iliyojaa upendo kwa rafiki yao mgonjwa, pia aliona mioyo yao iliyojaa imani kwa uwezo wake wa kuponya. Alipotazama godoro lile, alimwona mtu yule mwenye kupooza aliyekuwa na tamaa ya kuponywa ugonjwa wake. Tena, Yesu aliona mengi zaidi ya hayo. Aliona moyo wa mtu yule mwenye kupooza ukitamani jambo lingine zaidi kuliko kuponywa mwili wake peke yake.

Mtu yule mwenye kupooza wala marafiki zake wanne hawakusema hitaji lao, lakini Yesu alilijua hitaji hilo hata kabla ya wao kumweleza. Katika hali ile ya ukimya Yesu alitoa jibu moja dhahiri kwa hitaji lao. Alimwambia mtu yule mwenye kupooza, "Jipe moyo mkuu, mwanangu." Watu waliokuwamo mle ndani ya nyumba walimtumainia Yesu kumponya mgonjwa yule. Lakini Yesu alisema jambo ambalo hawakutazamia--jambo ambalo liliwashtua viongozi wa dini, watu waliokuwamo mle chumbani. Kwa kujua kwamba ilikuwa lazima kutimiza hitaji la kiroho kwanza, Yesu alimwambia yule mwenye kupooza kwa sauti ya huruma, "Mwanangu;

umesamehewa dhambi zako.”
(Mathayo 9:2)

Waandishi waliposikia maneno hayo walikasirika sana. Walifikiri, “Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye, Mungu?” (Marko 2:7) Walikuwa na hasira sana!

Yesu anajua kila kitu. Alijua mambo ambayo viongozi wale wa dini walikuwa wakifikiri. Alijua kwamba hawakutaka kukubali ukweli ya kwamba yeye alikuwa Mwana wa Mungu, na kwamba alikuwa na uwezo wa kusamehe dhambi. Yesu alithibitisha ukweli huu mbele yao lakini wao walikataa kuamini mambo yale waliyoyaona. Viongozi wale wa dini hawakusema mambo waliyokuwa wakifikiria, lakini Yesu aliyajua mambo hayo, akawauliza, “Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu? Kwa maana rahisi ni ipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi.” (Mathayo 9:4-6a)

Kisha Yesu alimgeukia mtu yule mwenye kupooza, akamwambia, “Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako.” (Marko 2:11) Mwenye kupooza alifanya kama Yesu alivyosema. Watu walistaajabu sana walipomwona akiketi na kisha kusimama kwa miguu yake. Aliinama na kukunja godoro lake na kulichukua na kisha akaondoka mle chumbani. Uso wake ulikuwa wenye furaha wakati alipokuwa akimtukuza Mungu kwa sauti kubwa kwa kila hatua aliyotembea. Watu wote walistaajabu,

wakamtukuza Mungu wakisema, “Namna hii hatujapata kuona kamwe.” (Marko 2:12).


Hakuna mtu ye yote anayeweza kuponya kiroho na kimwili isipokuwa Yesu Kristo pekee.

KAZI YA KUFANYA:

Yesu anaweza, tena ana nia ya kutusamehe dhambi zetu na kutusaidia katika shida zetu. Jaza maneno yanayokosekana ili kukamilisha sentensi zifuatazo.

(Chumba) kilijaa watu wengi. Watu wengine walitaka kumkaribia (Yesu). Walitoboa (tundu) darini, wakamtelemsha (rafiki) chumbani mbele ya Yesu.

Yesu (alisamehe) dhambi za mtu yule mwenye kupooza, aka(ponywa) mwili wake. Mtu yule mwenye kupooza (alimtukuza) Mungu wakati alipokuwa akienda zake.



Katika picha hii inayoeleza hadithi yetu ya Biblia, tunamwona Yesu akizungumza na mtu yule mwenye kupooza. Andika maneno ambayo

Yesu alimwambia kwanza. ("Jipe moyo mkuu, mwanangu. Umesamehewa dhambi zako.")

Kisha Yesu alimwambia mtu yule mwenye kupooza maneno gani? ("Ondoka, ujitwike kitanda chako uende nyumbani kwako.")

Katika Mathayo 9:2 tunasoma kuhusu uwezo wa Yesu juu ya dhambi. Andika herufi "K" kando ya sentensi ya kweli.

(K) Marafiki za mtu yule mwenye kupooza walikuwa na imani katika uwezo wa Yesu wa kuponya.

— Haikuwapasa kutoboa tundu darini.

(K) Mtu yule mwenye kupooza alihitaji kuponywa kiroho kwanza.

— Yesu hakuhusika na hitaji la kimwili la mtu yule mwenye kupooza.

(K) Baada ya mtu yule mwenye kupooza kuponywa, alimsifu Mungu.

(K) Yesu anajua fikira zetu kabla hatujasema.

Chora mstari kutoka kwa kila andiko lililo upande wa kushoto hadi kwa kila sentensi iliyo upande wa kulia ambayo inaeleza juu ya andiko hilo.

Mathayo 9:2 Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako.

Marko 2:2 Yesu aliona imani yao.

Marko 2:5 Alikuwa akisema nao neno lake.

Marko 2:10 Umesamehewa dhambi zako.

Luka 5:24 Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

1 Yohana 1:9

Mungu hutimiza ahadi yake siku zote. Tuna mojawapo ya ahadi kuu za Mungu katika kifungu hiki chetu cha kukumbuka.

Sisi sote tumetenda dhambi na tunahitaji msamaha wake. Lakini kwanza ni lazima kutubu dhambi zetu kabla ya kusamehewa. Kutubu si kubaya. Mungu ni mwaminifu na mwenye haki na ameahidi kutusamehe dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote kama tukiungama kwake.

Labda inaweza kuonekana kuwa si rahisi kutubu dhambi zetu. Tunajaribiwa kuchelewa kutubu dhambi zetu kwa muda mwingi sana. Baada ya kutubu dhambi zetu tunakuwa na amani mioyoni mwetu.



WAKATI WA KUFUNGA:

Mfalme Daudi alipotenda dhambi miaka mingi iliyopita, aliomba hivi: “Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu.... Unirudishie furaha ya wokovu wako.”

(Zaburi 51:10,12) Mfalme Daudi hakuwa na furaha mpaka alipotubu dhambi zake kwa Bwana na kupokea msamaha. Sisi pia hatuwezi kuwa na furaha halisi mpaka tunapotubu dhambi zetu na kupokea msamaha wa Mungu.

Tunapofunga somo hili, na tuimbe wimbo usemao, “Yesu Kwetu ni Rafiki,” kisha tuombe tukimshukuru Mungu kwa upendo wake wa kusamehe dhambi kwa kumtuma Yesu ulimwengu ni kuwa Mwokozi wetu.

WAKATI WA HUZUNI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 7:11-17

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Je! unafurahi? Mwamini Mungu ili akusaidie kuwa na furaha. Hali yako ya furaha itakuwa na mvuto mkubwa kwa vijana unaofundisha.

Wakati unapofundisha somo hili, utapata nafasi ya kuwakaribisha wanafunzi wako kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao. Kuwa tayari kwa maswali wanayoweza kuuliza na utoe majibu yatakayoridhisha njaa yao ya kiroho au tamaa ya kutaka kumjua Kristo.

Usisahau akilini mwako ya kwamba kwa sababu Yesu alimfufua mtu huyu katika wafu hatatoa kila shida inayotusumbua. Hebu fikiri kwa muda. Yesu aliona maombolezo mengine mengi katika miaka mitatu aliyokuwa akitenda kazi ya Mungu hapa ulimwenguni. Lakini tunasoma tu kuhusu nyakati tatu alipowafufua watu katika wafu: (1) Alipomfufua binti ya Yairo, Marko 5:21-43, (2) alipomfufua Lazaro, Yohana 11:30-44, na (3) alipomfufua mwana wa mama mmoja ambayo inasimulia katika somo hili letu. Yesu hakujaribu kuwafufua watu wote waliokufa, wala hakujaribu kumaliza magonjwa yote na mateso.

Katika mafunzo yako na matayarisho ya kufundisha somo hili, utaona ya kwamba katika mambo hayo Yesu alionyesha jinsi Mungu anavyowaza juu ya mateso yetu.

Mungu anaweza kutuondolea taabu au anaweza kutusaidia katika taabu. *Kuwa na kusudi la kuwafundisha wanafunzi wako ya kwamba Mungu atatusaidia katika nyakati zote za mahitaji.*

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu, Mwana mpendwa wa Mungu, alithibitisha ulinzi na msaada wa Mungu kwa wale walio na hitaji.
2. Mungu hatuahidi kwamba hatutakuwa na taabu, lakini anaahidi kuwa pamoja nasi wakati wa taabu.
3. Huruma ni jambo muhimu zaidi kuliko kusema tu "pole." Ni kuwa na moyo wa kuwaza hasa na kutaka kusaidia.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Sema:) Kila mtu amekwisha kuwa na jambo ambalo lilimfanya kuwa na huzuni. Kila mtu atakuwa na hali kama hiyo ya huzuni siku zijazo. Mungu hajasema ya kwamba tutakuwa na furaha wakati wote tutakapoishi hapa duniani. Lakini Mungu anatupenda sana hata anaahidi kuwa pamoja nasi wakati wa huzuni. Katika somo hili tunajifunza juu ya upendo na huruma ya Yesu kwa mama mmoja mjane aliyekuwa na huzuni nyingi.

Katika barabara yenye mavumbi iliyotoka katika mji wa Naini kuelekea upande wa mashariki palikuwa na mafuatano ya watu. Watu hao walikuwa wakilia na kuomboleza kana

kwamba jambo fulani baya sana lilikuwa limefanyika.

Katikati ya mafuatano ya watu wale palikuwa na watu wanne waliobeba machela (kitanda cha kuwabebea wagonjwa) mabegani mwao. Katika machela hiyo mlilazwa maiti ya kijana aliyekuwa amekufa. Alikuwa amekufa saa chache tu zilizopita. Kijana huyu alikuwa mwana pekee wa mamaye ambaye alikuwa mjane na ambaye sasa hakuwa na mtu ye yote wa kumpa maishilio. Alikuwa akitembea mbele ya jeneza la mwanawe akilia machozi mengi.

(Uliza:) Je! ilikuwa kosa kwa mama yule mjane kulia wakati kama huu?

(Sema:) La, si vibaya kuonyesha huzuni kwa kulia ikiwa mtu ana huzuni hasa.

Katika wakati huu wa aduhuri mafuatano ya watu wale walitembea kupitia mlango wa mji kuelekea makaburini kwa maziko. Mbele ya mafuatano ya watu wale palikuwa na wapiga zomari ambao walifuatwa na wanawake wa kuomboleza. Wanawake hawa walijiriwa kuomboleza. Wanawake hawa walifuatwa na marafiki. Kisha nyuma ya marafiki hawa kulikuwa na watu wote ambao kulingana na desturi walijiunga na mama yule mjane kushiriki naye huzuni yake.

Mafuatano ya watu wale walikutana na watu wengine waliokuwa wakitembea barabarani kuelekea mjini. Kwa mavumbi ya miguu yao na kwa jasho lao, ilikuwa wazi kwamba watu hao walikuwa wametembea maili nyingi. Wote walikuwa wamechoka

baada ya kutembea maili ishirini na tano kutoka Kapernaumu. Walikuwa wakijiharakisha kufika mjini Naini kabla usiku kuingia.

Watu hao walisimama ili kuwapisha mafuatano ya watu wale kupita. Walikusanyika upande mmoja wa barabara wakati wapiga zomari walipokaribia. Watu hao walikuwa wakimfuata Yesu.

Yesu alitazama wakati mafuatano ya watu wale walipokaribia mahali pale alipokuwa. Kisha mama yule mjane na watu waliokuwa wakibeba jeneza walipokaribia, Yesu alimwendea mama yule mjane. Uso na sauti ya Yesu zilionyesha huruma aliyokuwa nayo moyoni mwake. (Labda utapenda kufundisha kifungu cha kukumbuka hapa.) Kwa sababu Yesu anajua kila kitu hata jambo ambalo watu wanafikiri, alijua huzuni kuu mama yule mjane aliyokuwa nayo.

Yesu alimwambia mama yule mjane kwa upole na kwa huruma, "Usilie." Halafu alikaribia, akaligusa jeneza la mwana yule. Watu waliokuwa wakibeba jeneza hilo walisimama.

Yesu alisema na maiti ya kijana yule, akimwambia, "Kijana, nakuambia, inuka." Kwa hakika Yesu alikuwa akimwita kijana yule maiti kurudia uhai wake.

Maiti ya kijana yule ambaye alikuwa amefungwa kwa sanda aliinuka, akaketi. Alifunua mdomo wake, akaanza kusema. Yesu akampa mama yake. Watu wote waliokuwa katika mafuatano yale, na wale waliomfuata Yesu kutoka Kapernaumu walishikwa na hofu na mshangao. Walimwona

Yesu akionyesha uwezo wa Mungu juu ya mauti. Waliona ulinzi na huruma yake kwa watu wenye hitaji.

Katika mshangao mkuu, watu wale walimsifu Mungu wakisema, “Nabii mkuu ametokea kwetu” na “Mungu amekuja kuwaokoa watu wake.”

Hakika Mungu amekuja kuwaokoa watu wake, kutuokoa sisi katika dhambi zetu. Kama tukitubu dhambi zetu na kumwamini Yesu, tutaokolewa. Yesu hutupenda.

KAZI YA KUFANYA:

Huruma ni jambo muhimu zaidi kuliko kusema tu, “Pole.” Ni kumfikiria mtu hasa na kutaka kumfanyia kitu cha kumsaidia. Soma tu hadithi hii na andika maneno ambayo tulikosa kuandika badala yake.

Yesu na wanafunzi wake walitembea katika barabara kwenda kwa mji ulioitwa Naini. Walipokaribia mlango wa mji walisikia watu wakilia. Mwana pekee wa mama mmoja mjane alikuwa amekufa. Yesu alimhurumia, akamwambia, “Usilie.” Yesu alimfufua mwana yule akawa mzima tena.


Inatupasa kumsifu Mungu. Watu wale walipokwisha kumwona Yesu alimfufua kijana yule, walimsifu Mungu. Andika maneno waliyosema katika sifa zao.

Nabii mkuu ametokea kwetu

na

Mungu amekuja kuwaokoa watu wake.

Mungu amekwisha kutwambia kupendana sisi kwa sisi. Kata mojawapo ya sentensi hizo za kumalizia ambayo hailingani na sentensi hiyo iliyo ndani ya alama ya ufunguo.



furaha.
kutokuwa na shida?
ushirika na Mungu.
kuishi kwa amani na wengine.

Katika maandiko yetu ya Luka 7:11-17, tafuta vifungu vinavyotoa maneno yafuatayo na kuandika namba za vifungu hivyo katika visanduku.

Kifungu cha (12) kinasema kwamba kijana yule alikuwa mwana pekee wa mama mmoja mjane.

Kifungu cha (14) kinasema ya kuwa Yesu alisema, “Kijana, nakuambia, Inuka.”

Kifungu cha (11) kinataja jina la mji ule.

Kifungu cha (16) kinasema kwamba watu wote walimtu-kuza Mungu.

Labda utaulizwa maswali haya wakati mwingine. Andika (NDIYO) au (HAPANA) kama majibu yako kwa maswali haya.

1. Je! Wakristo watakuwa na wakati bila furaha? (Ndiyo)
2. Je! Mungu huponya magonjwa yetu yote? (Hapana)
3. Je! Yesu huwaonea huruma watu wenye huzuni siku hizi? (Ndiyo)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Kama vile Baba alivyonienda mimi, nami nilivyowapenda niñyi, kaeni katika pendo langu.”

Yohana 15:9

Mungu alimpenda Mwanawe pekee, lakini alimtoa kufa msalabani. Alifanya

hivyo kwa sababu anatupenda sisi. Anatutaka sisi kuokolewa kutokana na hukumu ya milele. Yesu alitupenda sana hata akatoa uhai wake kwa ajili yetu. Amekwisha kutufanyia mambo mengi sana hata tunaweza kuendelea kukaa katika upendo wake. Tunapoendelea kukaa katika upendo wake, tutakuwa na amani mioyoni mwetu hata wakati wa huzuni.

WAKATI WA KUFUNGA:

Tukiwa na huzuni au taabu ikitujia wiki hii tujaribu kufanya mambo yafuatayo:

- (1) Tukumbuke ahadi za Mungu,
- (2) Tuwatafute Wakristo imara kutusaidia,
- (3) Tuwe wavumilivu na kumwamini Mungu,
- (4) Tutafute jambo la kushukuru,
- (5) Tumsaidie mtu mwingine.

Omba ukimshukuru Mungu kwa upendo wake wenye huruma.

WAKATI TUNAPOPATWA NA MAMBO YA GHAFULA

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 14:22-33; Marko 6:45-52; Yohana 6:15-21

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Labda mtoto anaweza kusema kwamba haogopi kitu cho chote, lakini kwa kweli anaogopa kitu. Inaweza kuwa kwamba anaogopa giza, au mbwa, au wanyama wa mwitu, au nyoka, au milima, au kukaa peke yake, au moto au wizi.

Fikiri juu ya maswali haya wakati unapojitayarisha kufundisha. Je! Mungu anatosha wakati wa kuogopa? Anatusaidiaje wakati jambo la ghafula linapotupata?

Kusudi: Yesu anatumfundisha kwamba Mungu ni Baba wa upendo atakayesimama imara upande wa watoto wake wanaomwamini na kumtii. Mungu atatupa nguvu ya kukabili jambo lo lote la ghafula na rehema ya kuivumilia, au atatuondolea taabu. Wajibu wetu ni kumtegemea kabisa.

Labda utataka kusoma juu ya nyakati fulani katika siku za Biblia ambapo Bwana alionyesha uwezo wa Mungu. Soma Mathayo 19:26 na Mathayo 28:18. Soma Yohana 1:9 kuona ya kwamba Mungu yupo pamoja nasi kila mahali tuendako, na Zaburi 46:1 inayotwambia kwamba Mungu yuko tayari kila siku kutusaidia. Soma Mithali 3:5,6. Tukiamini kwamba mungu ana uwezo, na tukimwamini

kuwa pamoja nasi kutusaidia, basi tutamtegemea yeye kutupa msaada. Imani ni kuamini jambo kuwa kweli. Wasaidie wanafunzi wako kumwamini Yesu kabisa.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu, ambaye ni Mwana wa Mungu, mwenye uwezo, alionyesha uwezo wa Mungu wa kutusaidia kama tukimwamini.
2. Tunaweza kumtegemea Mungu kabisa kutusaidia wakati tunapopata na mambo ya ghafula.
3. Kwa kuwa Wakristo maana yake si kwamba hatutapatwa na taabu au mambo ya ghafula. Maana yake ni kwamba tunaweza kupokea nguvu na msaada wa Mungu wakati tunapopata taabu.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Sema:) Woga wengine ni wa maana na wengine huleta madhara.

(Uliza:) Je! kuna kijana ye yote anayeweza kutwambia wakati woga huwa wa maana? (Jibu ni kwamba, kama kuna hatari hasa, woga hutuzuia kufanya mambo ya kipumbavu.)

(Uliza:) Je! ni wakati gani ambapo woga huleta madhara? (Jibu ni kwamba, tukiogopa zaidi kupita kiasi, na woga kutuzuia kufanya jambo vizuri, basi woga huo utatuletea madhara.)

(Uliza:) Je! una woga wo wote, kama kuogopa milima, au giza au wanyama, au kuwa peke yako, au moto, au dhoruba, au watu wa hatari?

(Sema:) Vile Yesu alivyoonyesha kwa matendo yake kwamba Mungu ni mtakatifu, mwenye kusamehe, na mwenye upendo, ndivyo alivyoonyesha kwamba Mungu ana uwezo mwingi wa kutusaidia kukabili jambo lo lote linaloweza kutupata kwa ghafula. Katika somo hili tunajifunza juu ya wakati mmoja ambapo Yesu alionyesha uwezo mkuu wa Mungu.

Wanafunzi wa Yesu hawakuwa na wazo la kuvuka bahari kwenda Bethsaida. Yesu ndiye aliwaamuru kuingia ndani ya mashua na kuondoka kumwacha peke yake. Katika siku ile yote alishughulika na kufundisha, kuponya, na kuwalisha makutano ya watu waliokusanyika kwake. Kwa sababu ilikuwa jioni sasa, alitaka kuwaaga makutano ya watu wale kwenda zao nyumbani ili angeweza kubaki peke yake na Mungu. Basi aliwaaga wanafunzi wake baada ya makutano ya watu wale kuondoka, akapanda mlimani kuomba.

Usiku ulipoingia upepo ulianza kuvuma. Wakati huu wanafunzi walikuwa baharini na upepo ulizidi kuvuma sana. Walijaribu kuifanya mashua isitaabike kwa mawimbi. Baadaye kidogo walianza kuzuia mashua, kuzama. Upepo uliendelea kuvuma na mawimbi yalizidi kuwa makubwa na ya hatari.

Walishughulika kwa saa nyingi wakachoka. Walitamani kwamba kama Yesu angalikuwapo pamoja nao

ingalikuwa vema. Siku moja hapo zamani, wakati Yesu alipokuwa akilala ndani ya mashua yao walipokuwa wakivuka bahari, dhoruba ilitokea baharini. Kwa kuogopa kwamba wangekufa, walimwamsha Yesu, Yesu akatuliza bahari kwa kukemea upepo akisema, "Nyamaza, utulie." Lakini wakati huu Yesu hakuwapo pamoja nao. Au alikuwa nao?

Ilipokuwa karibu kupambazuka, Yesu alitazama bahari kutoka mlimani pale alipokuwa akiomba usiku kucha. Alijua ya kwamba marafiki zake (yaani, wanafunzi wake) walikuwa katika shida kubwa. Alianza kuwaendea akitembea juu ya maji.

Wakati wanafunzi wake walipomwona akiwajia kwa kutembea juu ya maji, waliogopa sana. Woga huu wao ulishinda hata ule wa dhoruba. Walidhani ya kuwa ni kivuli. Kisha walisikia sauti ikiwaambia, "Jipeni moyo; ni mimi. Msiogope." (Mathayo 14:27)

Kisha Petro alipaza sauti yake, akamwambia, "Bwana ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji." Akasema, "Njoo." (Mathayo 14:28-29a)

Petro alishuka mashuani. Alienda kwa miguu juu ya maji huku akimwangelia Yesu.

Mara Petro alitambua jambo alilokuwa akifanya. Alikuwa mbali na mashua na hapakuwa na kitu cho chote cha kushika. Upepo ulivuma kwa nguvu sana hata hakuweza kusimama, na mawimbi yalianza kumtupa huku na huku. Petro aliongopa sana. Alianza kuzama majini. Alilia kwa kusema,

“Bwana, niokoe.” Alijaribu kujizuia kuzama.

Mara Yesu alinyosha mkono wake, akamshika, akamwambia, “Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka?” (Mathayo 14:31) Wote wawili walitembea juu ya maji kwenda kwa mashua, kisha wakaingia ndani. Upepo ulikoma, kukawa shwari tena.

Wanafunzi walimwambudu Yesu katika mshangao mkuu wakisema, “Hakika wewe u Mwana wa Mungu.” Uwezo mkuu wa Mungu wa kukabili mambo yanayotokea kwa ghafula ulidhihirishwa machoni pao. Hawangekuwa na shaka hata kidogo kama Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Kama ishara ya itiko lao, walimwabudu Yesu.

Kama Yesu alivyomwambia Petro kumwendea ndivyo anavyotwambia sisi pia kumwendea hata kama kwanza inaonekana kuwa ni vigumu kufanya hivyo. Kwa Mungu mambo yote yanawezekana. Tunapomwendea Yesu tukifahamu ya kuwa yeye ni mwenye nguvu, na kwamba sisi ni wadhaifu, tunapata amani. Tunaondolewa woga wetu. Tunaweza kumtegemea yeye kabisa.

KAZI YA KUFANYA:

Wakati mwingine tunahitaji kuwa peke yetu na Mungu kumwomba. Andika majibu ya maswali haya yaliyo katika picha.



Je! ni nani waliokuwa ndani ya mashua wakati wa dhoruba? Wanafunzi.



Je! ni nani aliyekuwa mlimani akiomba? Yesu.

(Wanafunzi)

(Yesu)

Taabu zinaweza kutujia, lakini haitupasi kuwa na mioyo ya kutaabika. Chagua maneno ya kweli katika orodha ya maneno yafuatayo na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa ili kukamilisha sentensi hizo.

mashua	kuomba	upepo
usiku	imani	maji

1. Yesu alitaka (kuomba).
2. Wanafunzi waliingia ndani ya (mashua).

3. Kulivuma (upepo) wa mbisho.
4. Yesu alitembea juu ya (maji).
5. Ilikuwa wakati wa (usiku).
6. Petro alikuwa na (imani) haba.

Imani na woga hazipatani. Andika neno “NDANI” au uandike “NJE” kwenye milango hiyo pichani.

Woga unapoingia ndani.

Imani inaondoka nje.



Imani inapoingia ndani.

Woga unaondoka nje.



Sentensi hizi ziliandikwa kutoka kwa Mathayo 14:22-33. Chora mviringo kwa namba moja ya kifungu ambacho ni cha kweli.

Alipanda mlimani peke yake kuomba.

(23, 24, 25)

Usiogope.

(26, 27, 28)

Alisema, “Njoo”

(27, 28, 29)

Bwana, niokoe.

(29, 30, 31)

Mbona uliona shaka?

(30, 31, 32)

Hakika wewe u

Mwana wa Mungu.

(31, 32, 33)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako, nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.”

Isaya 41:10

Je! unaamini kwamba Mungu ana uwezo wote? Ikiwa unaamini hivyo, basi hupaswi kuogopa wakati unapopatwa na jambo la ghafula. Tuna hakikisho kamili ya kwamba Mungu yupo pamoja nasi, na kwamba hutupa nguvu wakati tunapomwomba. Kariri kifungu cha kukumbuka ili uweze kukumbuka ahadi ya Mungu wakati unapopatwa na jambo la ghafula.

WAKATI WA KUFUNGA:

Funga kwa maombi.

NJIA YA PEKEE KWA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 3:2-20;
Yohana 1:19-28; Luka 7:18-23

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Mungu alimchagua Mwanawe kuwa njia ya pekee ya kumwendea. Tunataka wanafunzi kujua ukweli huu. *Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba Mungu anaweza kutupokea tukiwa na imani katika Yesu Kristo.* Wanafunzi wakimjua Kristo wao binafsi, watataka kumshiriki na wengine.

Soma tena maandiko yote kisha uanze kujifunza kila kifungu. Mtambue Yohana kama yule aliyechaguliwa kumtayarishia Kristo njia. Yohana alijifunza maandiko ya Agano la kale kuhusu jinsi Kristo angekuwa. Soma tena Yeremia 23:5,6. Maelezo ya andiko hili yalimfanya Yohana kufikiri ya kwamba Yesu angekuja kama mfalme ambaye angewahukumu watu. Yohana aliona dhambi nyingi ulimwenguni na aliwaza moyoni mwake ya kwamba Yesu angebadilisha dhambi hizo. Hebu fikiria jinsi mfungwa (Yohana) aliyekuwa gerezeni alivyotaka sana kumwona Yesu akija katika uwezo wake mkuu.

Sasa soma Luka 7:1-23. Vifungu hivi vinakuonyesha mambo ambayo Yesu alikuwa akishughulika kufanya. Kuanzia kifungu cha 18 tunaona jinsi wanafunzi wa Yohana walivyomletea habari kuhusu mambo yote ambayo Yesu alikuwa akifanya. Yohana aliwatuma wanafunzi wake kwa Yesu kumwuliza kama yeye ndiye yule

waliyemtazamia kuja. Yesu alikuwa akifundisha na kuhubiri upendo na Yohana alitaka kuhakikisha kama yeye ndiye aliyekuwa Kristo kweli.

Kwa mambo hayo yote, wasaidie wanafunzi wako kuona kwamba Yesu ndiye Njia, na Kweli, na Uzima.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Mungu alimchagua Mwanawe kuwa njia ya pekee ya kumwendea.
2. Inatupasa kufahamu ya kwamba watu hawawezi kamwe kupokelewa na Mungu bila kuwa na imani ya kibinafsi katika Yesu Kristo.
3. Tuwe na nia ya kushiriki wokovu wetu na wengine.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Unaweza kuanza somo hili kwa hadithi hii.)

Palikuwa na mtu mmoja aliyetwa Petro ambaye alifanya kazi porini kujenga barabara. Kazi yake ilikuwa kuwatangulia watenda kazi wengine na kuweka alama ambapo barabara mpya ingefuata. Hata siku moja, Petro alifunga vyombo vyake vya kazi akaanza kurejea kwa wenzake kwa kupitia porini. Alitembea haraka porini kwa sababu alisikia njaa, lakini yeye hakuwa amebeba chakula.

Ilipoanza kuwa giza, Petro alitambua kwamba alikuwa amepotea. Kwa kupanda mlima mwingine aliwatafuta wenzake. Hakuona kitu. Hakujuu

mahali pale alipokuwa. Alitambua ya kwamba dira aliyokuwa akitumia kumwongoza ilivunjika.

Nchi ilianza kuwa baridi na upepo ulivuma. Petro hakuwa na chakula wala maji. Dira yake ilivunjika kwa hivyo hakuweza kupata njia ya kurejea kwa wenzake. Baada ya kutangatanga porini kwa siku tano akijaribu kutafuta njia ya kumrejesha kwa wenzake, hakuwa na nguvu ya kuweza kuendelea kujaribu. Jambo ambalo angeweza kufanya lilikuwa ni kufunga shati lake nyeupe kwa tawi la mti uliokuwa karibu na kutambaa kwenda kujificha katika mahali pa salama.

Petro alikuwa karibu kufa wakati watu waliokuwa wakimtafuta walipompata siku ya pili yake. Alifurahi sana kuongozwa na watu wale kutoka mle porini.

(Uliza:) Je! kuna wakati unapotaka kufanya mambo katika njia yako mwenyewe, au unafuata maongozi? Je! unayo "dira" ya kukuongoza maishani mwako? Je! una kitu cha kukuonyesha jinsi ya kuishi? Je! una kitu cha kukuonyesha njia ya haki?

(Sema:) Tunayo "dira" kwa maisha yetu. Ni Yesu Kristo. Atatuongoza kutoka katika pori ya dhambi na kutuonyesha njia ya haki.

(Uliza:) Je! kuna njia nyingi ya kumwendea Mungu au kuna njia moja tu ya haki ya kumwendea? (Njia moja tu.)

(Sema:) Yohana atatuonyesha jinsi kumsikia Mungu akisema kulimfanya kupata njia ya pekee kwa Mungu.

Yohana ambaye maishani mwake alikuwa mtu shujaa wa nyikani alitembea katika nchi iliyokuwa kando ya Mto wa Yordani akiwaita watu kuja kutubu dhambi zao. "Geuzeni njia zenu mbatizwe," aliwahubiri watu. "Mungu atawasamehe dhambi zenu." (Soma Luka 3:3)

Makutano ya watu walikusanyika kusikiliza mahubiri ya Yohana, mhubiri wa ajabu. Aliwauliza watu kwa sauti thabiti, "Ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? ...Shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni." (Luka 3:7b,9)

Watu walikuwa bado kusikia mahubiri kama haya. Walistaajabu kama Yohana alikuwa Masihi au la. Baadhi ya viongozi wengine wa dini Yerusalemu waliwatuma watu kwa Yohana kumwuliza kwamba, "Wewe u nani?" (Soma Yohana 1:20-23.) Yohana alitoa jibu hili.

Siku moja, Yohana alimdhihirishia Mfalme Herode dhambi zake. Yohana alifungwa gerezeni kwa sababu hii. Wakati Yohana alipokuwa gerezeni alisikia kwamba Yesu alikuwa akiwavuta watu wengi kwake. Hii maana yake ilikuwa kwamba Masihi alikuwa amekuja.

Yohana alifikiri sana juu ya kazi ya kiongozi huyu mpya -- alifikiri juu ya ujumbe wake wenye nguvu uliopinga dhambi, mashambulio yake juu ya maovu ya Shetani, na ushindi wake wa mwisho wa kupinga dhuluma za namna zote.

Badala ya fikira hizo za Yohana, Yesu alikuwa mwalimu maskini ambaye alitembelea miji na nchi ya Galilaya akiwa pamoja na wavuvi wachache. Alikwenda huku na huku akitenda matendo ya upendo ya kuponya na kuwafundisha watu habari za Baba yake aliye mbinguni. Je! ni kwa nini hakukaa tu Yerusalemu kuwapendeza viongozi muhimu wa dini? Wao ndio wangemsaidia kuwa na mvuto kwa nchi hiyo yote. Yohana alishangaa kwa sababu Yesu alikuwa akihubiri upendo na rehema ya Baba yake badala ya kuhubiri tu juu ya hukumu ya Mungu na juu ya dhambi.



Yohana alianza kuwa na wasiwasi. Je! alikuwa amehubiri vibaya? Je! alikuwa ametenda kosa? Je! Yesu alikuwa kiongozi mwingine tu mkuu?

Yohana aliwaambia marafiki zake, "Nendeni kwa Yesu mkamwulize kama yeye ndiye ajaye atatuonyesha njia ya kumwendea Mungu, au tumtazamie mwingine kuja."

Marafiki za Yohana walimwendea Yesu wakampata. Walimpata kama

amezungukwa na vipofu, viwete, wagonjwa, viziwi, wenye huzuni, maskini, na wenye shida. Watu hawa wote walikuwa wamekuja kwa Yesu wakitaka msaada. Marafiki wale waliokuwa waaminifu kwa bwana yao, Yohana, hawakusita kumwuliza Yesu swali.

(Soma Luka 7:20-23.) Katika maandiko haya tunaona jinsi marafiki wale walivyomwuliza Yesu kwamba alikuwa nani. Yesu aliendelea tu kufanya miujiza ya kuponya kisha aliwaambia kurejea kwa Yohana kumwambia mambo waliyoyaona, na kwamba yeye alikuwa nani.

(Uliza:) Je! unafikiri ya kwamba jibu la Yesu lilimridhisha Yohana?


(Sema:) Ndiyo, lilimridhisha kwa sababu alimwamini Yesu Kristo. Wakati tunapokuwa na shaka na kumwuliza Yesu kutupa jibu, ni lazima tuwe tayari kusikiliza jibu analotupa na kuliadini. Mara nyingi tunaweza kusoma Biblia zetu na kupata majibu ya maswali yetu. Kisha inakuwa wajibu wetu kusikiliza na kuamini.

(Sema:) Yesu alisema, 'Naye heri mtu ye yote asiye chukizwa nami.' (Luka 7:23) Maneno haya ndiyo yanapaswa kuwa mfano kwetu kufuata na kumwamini Kristo.

KAZI YA KUFANYA:

Njia ya kwenda kwa Mungu ni kama safari. Wakati unapojibu swali, chora mshale kwenye njia hiyo mpaka kwa swali lingine.

5. Je! una uchaguo? Yesu alizungumza juu ya njia mbili. Njia moja mwisho wake ni mauti ya milele. Njia nyingine mwisho wake ni uzima wa milele. Soma Mathayo 7:13-14. Una uchaguo. Je! unafuata njia ipi sasa?
4. Kwa nini huweza kupata njia ya kukuongoza kwa Mungu? Soma Isaya 53:6a. Halafu fikiria "Je! maana ya kugeukia njia yangu mwenyewe ni nini?" Je! umekwisha kugeukia njia yako mwenyewe?
3. Je! Mungu hukujali wewe? Soma Zaburi 139:1-6. Unajuaje ya kwamba Mungu hukujali? Kwa sababu anajua kila kitu ninafanya.
2. Je! Mungu anapendezwa na ulimwengu huu mdogo na watu waliomo ndani? Soma Zaburi 40:5. Kata maneno yaliyo katika alama hii () ambayo si kweli. Mungu huonyesha (~~miujiza yake juu ya viumbe~~) (upendeleo wake kwa watu) kwa kazi zake za ajabu hapa ulimwenguni na (~~mawazo yake juu yetu~~) (~~malaika mbinguni~~) ambayo hayawezi kuhesabiwa.
1. Je! Mungu yuko wapi? Soma Yeremia 23:23, 24. Je! unaweza kuonyesha mahali hasa ambapo Mungu yupo ulimwenguni, mwezini, au mahali po pote? Vifungu hivi vinasema "Mbingu na nchi hazikuja-wa nami?" Maana Mungu ni katika kila mahali.



Soma Mathayo 7:13, 14. Chora mstari kutoka kwa sentensi zilizo upande wa kushoto hadi kwa maneno yaliyo upande wa kulia ambayo yatazikamilisha.

Mlango (mwembamba) ulionyooka
Mlango mpana
Njia iliyonyooka ~~UZIMANI~~
Njia pana
Watu wengi ~~MAUTI~~
Watu wachache

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

**“Yesu akamwambia, Mimi ndimi
njia, na kweli, na uzima; mtu haji
kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.”**

Yohana 14:6

Ukitaka kumpata Mungu, kwanza
unahitaji NJIA. Ukitaka kumjua
Mungu, unahitaji UKWELI. Ukitaka
kumfurahia Mungu, unahitaji UZIMA.
Katika kifungu hiki, wasaidie
wanafunzi wako kujua kwamba Yesu

anawataka kumwendea. Watie
wanafunzi moyo kujiuliza wenyewe
swali hili “Je! Yesu anataka nifahamu
nini juu yake?” Kisha walijibu swali hilo
wao wenyewe. (Ya kwamba yeye ndiye
Njia, na Kweli, na Uzima, na kwamba
tunaweza kumwendea Mungu kwa
yeye.)

WAKATI WA KUFUNGA:

(Sema:) Kila mmoja wetu ana wajibu
wa kuchagua jinsi atakavyomwitikia
Yesu kama Njia ya pekee kwa Mungu.
Je! tutamwendea kwa kumpokea kama
Mwokozi wetu? Au hatutamwendea?
Waambie wanafunzi kufikiria jibu
kimya halafu kama wengi wao
watataka kueleza itiko lao, waruhusu
kufanya hivyo. Funga kwa maombi.

NJIA ISIYOPENDWA

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 6:25-40, 66-71

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Ili kufundisha somo hili, ni lazima kujifunza sura yote ya sita ya kitabu cha Yohana. Wakati unapojifunza sura hii, tafuta na kupata majibu ya maswali haya yafuatayo wewe mwenyewe. Je! ni kwa nini Yesu alikataa kufanywa kuwa mfalme na watu? Je! Yesu angetenda mambo mema zaidi kwa kuishi kama mfalme mkuu kuliko kufa kama mhalifu? Je! Wakristo wanaweza kupendwa na watu? Je! inanipasa kufanya nini kama marafiki zangu wakiniita kwa majina mabaya na kunidhihaki kwa sababu mimi ni Mkristo?

Kama una ubao wa kuandika, itakuwa msaada sana kuandika neno "Taji" upande mmoja na kuandika "Msalaba" upande mwingine. Unapofikia schemu hii ya somo, uandike chini ya "Taji" orodha ya mambo yote ambayo Yesu angalifanya kama angalikuwa mfalme ili kuwapendeza watu. Chini ya "Msalaba" andika orodha ya mambo ambayo Yesu alifanya kwa kutoa uhai wake msalabani.

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi wako kuona kwamba Kristo alichagua njia ngumu isiyopendwa kwa maisha yake ili kwamba waweze kupata wokovu kwa sababu ya kifo chake msalabani.

Chunguza maisha yako mwenyewe. Je! unajaribu kuishi kama Kristo alivyoishi? Je! unataka kupendwa na watu wa kanisa lako au na wanafunzi wako unaowafundisha au unajaribu kuishi kama Kristo anavyokuongoza kuishi? Ikiwa maisha yako ni mfano mzuri kwa wanafunzi hawa unaofundisha, basi bila shaka unaishi kama Kristo anavyotaka.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu alikataa mahimizo yote ya watu waliotaka kumfanya kuwa mfalme.
2. Yesu alimtii Baba yake kwa kutoa uhai wake ili sisi tuweze kupata uzima wa milele.
3. Ni lazima tuwe na lengo la kumfuata Yesu Kristo kwa kumpendeza Mungu kwanza hata kama kufanya hivyo kunaweza kutufanya tusipe ndwe na watu.

KULIFUNDISHA SOMO:

Simulia hadithi jinsi Yesu alivyowalisha watu 5,000 kama kiini cha somo hili. (Soma Yohana 6:1-14 na Marko 6:35-44. Sema:) Wanafunzi wa Yesu walikuwa wakitaka kusema naye. Walipanda mlimani, wakaketi pamoja na Yesu katika mahali pa faragha ili wangeweza kusema naye, lakini mkutano wa watu walimfuata Yesu. Yesu alianza kufundisha na kuwaponya watu. Ilikuwa ikikaribia kuwa usiku na wanafunzi wa Yesu walimwambia, "Uwaage watu hawa, ili waende zao

mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula.” (Marko 6:36) Yesu aliwajibu, “Hakuna haja ya kuwaaga. Wapeni ninyi chakula.”

Wanafunzi hawakuwa na chakula isipokuwa mikate mitano na samaki wawili wa mtoto mmoja aliyekuwapo pale. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwaketisha watu katika makundi kwenye majani, kisha alibariki mikate ile mitano na samaki wawili, akawagawia watu wote, wakala, wakashiba, wanafunzi wakakusanya vipande vilivyobaki vikajaza vikapu kumi na viwili. Mwujiza huu ulimfanya Yesu kupendwa sana na watu.

Watu walikuja tena siku ya pili yake kumtafuta Yesu. Watu hawa walistaajabia kazi ya Yesu ya ajabu. Hakika Yesu hakuwa mtu wa kawaida tu kwa sababu aliwalisha watu zaidi ya 5,000 na idadi hii haikuwa pamoja na ya wanawake na watoto waliokuwapo. Hakika Yesu alikuwa Masihi na mfalme ambaye manabii walihubiri juu yake. Angekuwa mfalme wa ajabu. Hangekuwa kama Mfalme Herode aliyechukiwa, ambaye alitumikia serikali ya Rumi na ambaye alikata kichwa cha Yohana Mbatizaji. Yesu akiwa kama mfalme angewaokoa Wayahudi hao kutoka mamlaka mabaya ya Herode, na kuwafanya huru kutokana na utawala wa Rumi. Angewaponya na kuwalisha na kuwapa mafanikio na amani.

Watu walizungumza kwa wasiwasi katika makundi kuhusu kumfanya Yesu kuwa mfalme wao. Mpango huu ulikuwa wa hatari, lakini wao waliona ya kuwa ulifaa. Yesu alijua tamaa zao

za kutaka kumfanya kuwa mfalme hata kabla ya wao kufanya kitu cho chote. Alijua jambo lingine zaidi ya kwamba kufanywa kuwa mfalme wakati huu haukuwa mpango wa Mungu. Hakika alikuwa Masihi lakini kusudi la Mungu lilikuwa ni kuwaokoa watu katika dhambi zao, wala halikuwa la kuwaokoa watu na maadui zao. Yesu alikuja kutoa uzima wa milele wala hakuja kutoa chakula cha daima.



Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kuwaambia makutano ya watu wale waliomfuata kurejea nyumbani. Kisha alipanda mlimani tena peke yake kuomba. Watu walikasirika sana! Kwa nini Yesu hakutaka kuwa mfalme?

(Uliza:) Je! kwa nini Yesu alipendwa sana na watu wengi hata wakamtafuta?

(Jibu:) Kwa sababu walikwisha kusikia au kuona miujiza yake ya kuponya.

(Uliza:) Je! ni kitu gani kilichomfanya Yesu kupendwa sana na watu hata wakawa tayari kufanya mapinduzi na kuhatarisha maisha yao ili kumlazimisha kuwa mfalme wao?

(Jibu:) Mwujiza ambao Yesu alifanya wa kulisha mkutano wa watu uliwashawishi watu kwamba angekuwa

mfalme wa ajabu ambaye angewalisha wakati wa njaa maishani mwao mwote.

(Uliza:) Je! ingalimpasa Yesu kufanya nini ili kuwapendeza watu?

(Jibu:) Kama angaliwaruhusu kumfanya kuwa mfalme.

(Uliza:) Je! ilimpasa Yesu kufanya nini ili kumpendeza Mungu?

(Jibu:) Ilimpasa kuchagua kufa msalabani.

(Uliza:) Je! Yesu angalifanya mambo mengi mema zaidi kwa kuishi kama mfalme mkuu kuliko kufa msalabani kama mhalifu? (Andika chini ya neno "Taji" orodha ya mambo yote ambayo Yesu angalifanya kama angalikuwa mfalme ili kuwapendeza watu. Chini ya neno "Msalaba" andika orodha ya mambo ambayo Yesu alifanya kwa kutoa uhai wake msalabani.)

"TAJI"

"MSALABA"

Angewaponya.

Aliandaa njia ya kumwendea Mungu.

Aliwalisha watu.

Aliondoa lawama za dhambi zetu.

Alifanya sheria nzuri.

Alitoa hukumu. Alifundisha habari za Mungu.

Alitoa maisha ya milele na msamaha wa dhambi zetu.

Aliwafariji.

(Uliza:) Je! Yesu alisema kwamba alitaka nini zaidi kuliko kupendwa? Je! kutenda mapenzi ya mtu maana yake nini?

(Jibu:) Kufanya jambo analotaka, kufuata maongozi yake.

(Uliza:) Je! maana ilikuwa nini Yesu kufanya mapenzi ya Baba yake?

(Jibu:) Kufa msalabani.

(Uliza:) Je! kama Yesu angalikuwa mfalme angalimsaidia nani?

(Jibu:) Watu walioishi wakati ule tu.

(Uliza:) Je! kama Mwokozi, Yesu angemsaidia nani?

(Jibu:) Watu wote wa nyakati zote.

Baadhi ya watu ambao Yesu aliwalisha mlimani walimfuata mpaka Kapernaumu. Yesu alijua sababu yao ya kumfuata. Aliwahukumu kwa sababu walifikiria zaidi juu ya chakula kuliko walivyomfikiria yeye Mwana wa Mungu. Lakini njia hiyo haikuwa ya kupendwa na watu. Watu waliomfuata kwa kusudi la kupata chakula cha bure hawakupendezwa wakati alipowaambia habari hizi za uzima wa milele badala ya kuwalisha.

Watu wengine walimfuata Yesu mpaka sinagogini wakamwuliza kwamba ni ishara gani ambayo angefanya ili wangeiona na kumwamini. Walimkumbusha Yesu ya kwamba Musa aliwapa babu zao mana jangwani.

(Sema:) Soma Yohana 6:32-40.

(Sema:) Katika Yohana 6:47-51, Biblia inaeleza jinsi alivyosimama imara kwa kazi ambayo Mungu alimtuma kuja kufanya ingawa kazi hiyo haikumfanya kupendwa na watu. Watu walianza kushindana wao kwa wao kuhusu jibu ambalo Yesu aliwapa. Yesu alikuwa amesema, "Mimi ndimi chakula cha uzima... Nilishuka kutoka

mbinguni... Yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa... Ye yote atakayekula mkate huu ataishi milele... Mkate nitakaotoa kwa maisha ya ulimwengu ni mwili wangu." Watu walianza kunung'unika. Walisema, "Awezaje mtu huyu kutupa sisi mwili wake ili tuule?" Jambo hili lilikuwa la ajabu sana kwao! Waliondoka na kumwacha Yesu.

Hata watu wengi waliojiita wanafunzi wa Yesu walisema, "Neno hili ni gumu." Hawakufahamu kwamba kumpokea Yesu kama Mwana wa Mungu aliyetoka mbinguni kungeendelea kuwapa uzima wa milele kama kupokea mkate kungeendelea kuwapa uzima wa kimwili. Wanafunzi hawa pia walikuwa wamepoteza tumaini lao kwa Yesu.

Wakati watu walipokwisha kuondoka na kuwaacha Yesu na wanafunzi wake kumi na wawili, Yesu aliwauliza wanafunzi hao kwa huzuni, "Je! ninyi nanyi mwataka kuondoka?"

Simoni Petro alimjibu, "Bwana! Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu." (Yohana 6:68-69)

Yesu ambaye alipendwa sana nchini kwa ghafula alibaki tu na wanafunzi wake kumi na wawili, na mmojawapo wa wanafunzi hao akawa msaliti wake.

KAZI YA KUFANYA:



1. Usifanye mambo kwa makusudi ya choyo au kwa kujigamba.



2. Watendee mema wale wanao-kukosea.



3. Usijaribu kuwaiga wale ambao si Wakristo.



4. Hubiri ili kumpendeza Mungu, siyo kuwapendeza watu.

Je! daima naweza kusema mambo ambayo yatanifanya kupendwa na watu?

Mtume Paulo alieleza mambo aliyotaribu kufanya sikuzote. "...ndivyo tunenavyo; si kama wapendezao wanadamu, bali wampendezao Mungu anayetupima mioyo yetu. Maana hatukuwa na maneno ya kujipendekiza wakati wote, kama mjuavyo... Hatukutafuta utukufu kwa wadamu..." (1 Wathesalonike 2:4-6)

Chagua mojawapo ya picha hizo (juu) ambayo inalingana na mambo ambayo Mungu anakuambia juu ya kujaribu kupendwa kwa mambo unayosema. Andika namba ya picha hiyo hapa (4).

Je! yanipasa kufanya mambo kwa kusudi la kuwafanya watu kufikiri kwamba mimi ni mkuu?

Wafilipi 2:3 inasema, "Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake."

Sasa chagua picha inayolingana na mambo ambayo Mungu anakwambia

kufanya katika kifungu hiki. Andika namba ya picha hiyo hapa (1).

Je! yanipasa daima kuwaiga rafiki zangu?

Katika Warumi 12:2 tunasoma: "Wala msiifuatishie namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."

Chagua picha inayolingana na mambo ambayo Mungu anakwambia kufanya katika kifungu hiki. Andika namba ya picha hiyo hapa (3).

Je! yanipasa kuwatendea nini wale wanaotaribu kunidhulumu?

"Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angaliani yaliyo mema machoni pa watu wote.... Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema." (Warumi 12:17,21)

Andika namba ya picha inayolingana na mambo ambayo Mungu anakwambia katika vifungu hivi (2).

Tazama picha zile tena wakati unapofikiria majibu ya maswali haya:

1. Je! yanipasa kuhubiri habari za Yesu kwa marafiki zangu hata kama hawataki kusikia habari zake? (Ndiyo)
2. Je! ni sababu zipi mbili mbaya ambazo ningekuwa nazo kwa kufanya jambo ambalo watu husifu? (Kwa pesa au kupendwa na watu)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

“Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.”

Wagalatia 1:10

Kumpendeza Kristo aliyekufa ili kukupa uzima wa milele ni muhimu zaidi kuliko kupendwa na mtu ye yote.

WAKATI WA KUFUNGA:

(Uliza:) Je! unafikiri ni haki kwa Mkristo kupendwa na watu?

(Sema:) Mkristo mwenye akili, ujuzi, na uwezo, ambaye anatumiwa na Mungu, anaweza kuwa maarufu na muhimu. Lakini kusudi analopaswa kuwa nalo ni kuweka mapenzi ya Mungu kwanza maishani mwake.

(Uliza:) Yesu alikubaliye kumpendeza Baba yake hali kufanya hivyo kungemfanya kutopendwa na watu na hata kutoa uhai wake?

(Sema:) Alimpenda Baba yake sana hata akataka kufanya kila kitu kumpendeza. Ukiwa Mkristo unaweza kumwomba Yesu kujaza upendo kama huo moyoni mwako na utampenda Mungu zaidi kuliko kitu au mtu ye yote.

(Uliza:) Jambo hili litakusaidiaje kujibu swali la kupendwa?

(Sema:) Nitaweka moyo wa kumpendeza Bwana mbele ya kuwapendeza marafiki zangu.

Omba pamoja na wanafunzi wako ili watamwomba Mungu kuwasaidia kuwa na upendo kama huu mioyoni mwao.

NI NJIA NGUMU WAKATI MWINGINE

MASOMO YA BIBLIA: Yohana 9:1-

41

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Ni muhimu kwako wewe kama mwalimu kusoma Yohana 9 yote mpaka ufahamu sawasawa hadithi iliyomo ndani. Sura hii inasimulia juu ya kipawa cha kuona, juu ya Yesu kukataliwa na watu, na juu ya upendo wa Kristo katika njia ambayo utataka kushiriki na wanafunzi wako.

Wanafunzi wako wanataka kujua kwa nini kila mtu humchukia mtu anayetenda mema. Wanataka kujua kwa nini Mungu humwacha Mkristo kuteswa bila kumlinda? Je! tunaweza kutazamia kuwa na shida ya namna gani kwa sababu ya ushirika wetu na Kristo? Mungu atatusaidia kwa jinsi gani? Je! inatupasa kuonyesha tabia zetu kwa jinsi gani wakati tunapodhulumiwa?

Wakati unapofundisha somo hili, kusudia kuomba ya kwamba Roho Mtakatifu atamfanya kila mmojawapo wa wanafunzi wako kutaka kuishi kwa moyo wazi kwa Mwokozi wake na kutegemea ahadi ya Mungu kumtia nguvu.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Watu wanaomfuata Yesu hukabiliwa na pingamizi kwa ajili ya imani yao.
2. Watu wanaomfuata Yesu wanaweza kutegemea uwezo wa Mungu kuwasaidia kusimama imara.

3. Kila mwanafunzi anaweza kutegemea ahadi ya Mungu kumtia moyo kuwa Mkristo wa kweli kwa Yesu wakati anapokabiliwa na pingamizi.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Sema:) Katika hadithi yetu ya leo tutaona ya kwamba mtu mmoja ambaye ni kipofu akutana na Yesu. Alijifunza kwamba kuwa upande wa Yesu kungewafanya watu wengine kuwa maadui zake.

Ulikuwa wakati maalum mjini Yerusalemu. Wayahudi walikuwa wakiadhimisha sikukuu ya furaha kuu - Sikukuu ya Vibanda. Katika hekalu kuu palikuwa na ibada maalum na nyimbo na umati wa watu walioandamana kuja kusujudia.

Lakini palikuwa na mtu mmoja ambaye hakuweza kuona rangi mbalimbali za mapambo au sherehe yenyewe. Alikuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake. Katika siku za juma aliketi kando ya njia. Aliwaomba watu waliopita pale kumpatia pesa kwa kusema, "Nisaidieni mimi maskini, mpate kubarikiwa."

Lakini wakati huu alikuwa amenyamaza kwa sababu ilikuwa siku ya Sabato. Siku hii hakuna mtu aliyetenda kazi wala waombaji pesa hawakuomba. Kipofu yule aliketi tu na kusikiliza kelele za watu wenye furaha na za watu waliompita pale njiani.

Kwa ghafula alimsikia mtu mmoja aliyekuwa karibu naye akiuliza, "Rabi,

ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?" (Yohana 9:2)

Mtu yule aliyeitwa Rabi (yaani, Mwalimu) alijibu, "Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi ya Mungu zidhihirishwe ndani yake." (Yohana 9:3)

Bila shaka kipofu yule alistaajabia maneno hayo ya ajabu. Yesu alikuwa na maana gani kwa kusema "kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake?"

Yesu aliendelea kusema, "Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana; usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi. Muda nilipo ulimwenguni mimi ni nuru ya ulimwengu." (Yohana 9:4,5)



Nuru ya ulimwengu! Kipofu yule alitaka sana kuona nuru. Yesu alitema mate chini, akafanya tope kwa yale

mate. Akampaka kipofu yule tope za macho. Kisha akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu." (Yohana 9:7)

Haikuchukua muda mrefu kabla ya kipofu yule kupapasa njia ya kwenda birikani. Kwa kupiga magoti kando ya birika, alinawa uso wake kuondoa matope, yale ambayo Yesu alimpaka. Alifumbua macho yake akaona kuta za mawe na watu waliokuwa wakitembea! Kwa wasiwasi mkubwa na furaha, alikimbia kwenda kuwatafuta wazazi wake na marafiki zake. Na zaidi ya hayo yote, alitaka kumwona Yesu. Majirani na marafiki zake waliulizana wao kwa wao, "Je! huyu siye yule aliyekuwa akiketi na kuomba?" (Yohana 9:8)

Wengine walisema, "Ndiye." Lakini wengine hawakuweza kuamini. Walisema, "La; lakini amefanana naye."

Lakini kipofu yule mwenyewe alisema, "Mimi ndiye." Kisha alisimulia habari juu ya Yesu na juu ya matope na juu ya kunawa uso wake birikani. Kila mtu alitaka kujua mahali ambapo Yesu alikuwapo lakini kipofu mwenyewe pia hakujua. Watu walimtaka kipofu yule kusimulia hadithi yake kwa viongozi wa dini. Mafarisayo walitaka sana kusikia jambo hili kwa sababu katika wiki iliyokuwa imepita walijaribu mara mbili kumwua Yesu lakini hawakufaulu. Walitangaza wazi ya kwamba mtu ye yote ambaye angeadhibiwa.

Mafarisayo hao walisikiliza kwa makini hadithi ya kipofu yule. Kisha walisema, "Kumbe Yesu alitema mate

chini akafanya tope!” Kitendo hiki kilithibitisha kwamba Yesu alivunja sheria ya Sabato kwa kufanya kazi. Tena alimpaka kipofu yule tope za macho. Hii ilikuwa hatia nyingine mbaya sana. Mafarisayo wengine walisema, “Mtu huyo hakutoka kwa Mungu kwa sababu haishiki Sabato.” Wengine waliuliza, “Awezaje mtu mwenye dhambi kufanya ishara kama hizo?” (Yohana 9:16).

Kabla ya kuendelea kumshtaki Yesu, viongozi waliwaita wazazi wa kipofu yule. Labda wazazi wale walikuwa wamekwisha kusikia habari kuhusu adhabu ambayo ingetolewa kwa mtu ye yote ambaye angemfuata Yesu. Kwa hivyo walijibu, “Tunajua ya kuwa huyu ndiye mwana wetu, tena ya kuwa alizaliwa kipofu; lakini jinsi aonavyo sasa hatujui; wala hatujui ni nani aliyemfumbua macho. Mwulizeni yeye mwenyewe; yeye ni mtu mzima; atajisemea mwenyewe” (Yohana 9:20-21).

Kisha Mafarisayo walimwambia mtu yule aliyekuwa kipofu, “Apa mbele ya Mungu kusema ukweli. Sisi tunajua ya kuwa Yesu ni mwenye dhambi.”

Waliendelea kumwuliza ili kuwaeleza jinsi mambo hayo yalivyopata kutukia. Aliwajibu, “Najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona.... Nimekwisha kuwaambia, wala hamkusikia; mbona mnataka kusikia tena? Ninyi nanyi mnataka kuwa wanafunzi wake?” (Yohana 9:25,27)

Kipofu yule hakutaka kukana mambo aliyokwisha kusema juu ya Yesu. Alisema, “Twajua ya kuwa Mungu hawasikii wenye dhambi; bali

mtu akiwa ni mcha Mungu, na kuyafanya mapenzi yake, humsikia huyo. Kama huyo asingalitoka kwa Mungu, asingeweza kutenda neno lo lote.” (Yohana 9:31, 33)

Maneno haya yaliwakasirisha viongozi sana, wakapaza sauti zao, wakasema, “Ama! wewe ulizaliwa katika dhambi tupu, nawe unatufundisha sisi?” (Yohana 9:34) Kwa maneno makali, Mafarisayo walimkamata kipofu yule, wakamtoa nje ya sinagogi.

Baada ya tukio lile, watu wangemtendea kipofu yule kama maiti. Wangekataa kusema naye au kula naye. Hawangemsaidia katika njia yo yote. Lakini palikuwa na mtu mmoja ambaye angemjali. Mtu ambaye angemtafuta na kuzungumza naye bila kujali mambo ambayo Mafarisayo wangefanya. Mtu huyu alikuwa Yesu. Alimwuliza kipofu yule “Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?”

Kipofu yule alimjibu, “Ni nani, Bwana, nipate kumwamini?”

Yesu alimjibu kwa upole, “Umemwona, naye anayesema nawe ndiye.”

“Naamini,” kipofu yule alisema, akamsujudia Yesu. Alitambua ya kwamba Nuru ya Ulimwengu (ambaye ni Yesu) ilikuwa nzuri zaidi kuliko nuru ya kawaida kwa macho yake.

(Uliza:) Je! kwa nini viongozi wa dini walimtoa kipofu yule aliyeponywa nje ya sinagogi?

(Sema:) Alikataa kukubali maoni yao ya uwongo kwamba Yesu alikuwa mwenye dhambi ambaye hangaliweza

kumponya. Aliamini kwamba Yesu alitoka kwa Mungu na kwamba alifanya kazi ya Mungu.

(Uliza:) Je! unafikiri kwamba ukimfuata Yesu watu watakutendea kama Mafarisayo walivyomtendea kipofu yule ambaye aliponywa na Yesu?

(Sema:) Ndiyo, unaweza kutendewa mabaya, hata hivyo utaweza kuonyesha imani yako katika Kristo kuwa kusimama imara.


(Uliza:) Je! utapata nguvu ya kusimama imara kwa ajili ya Yesu kutoka wapi hata kama uko taabuni au kama unateswa?

(Sema:) Soma kifungu cha kukumbuka kupata jibu lisemalo kwamba Yesu atakusaidia (Waebrania 13:5b, 6).

KAZI YA KUFANYA:

Kwa muda wa miaka mingi sana watu wamekuwa wakitumia ngao kujikinga nayo. Mkristo pia ana ngao. Ngao yake ni imani. (Waefeso 6:16) Mkristo anapoamini upendo na uwezo wa Mungu, anaweza kukabili shambulio lo lote.

Mungu anawaambia Wakristo dhahiri katika Neno lake jinsi wanavyopaswa kuonyesha matendo yao wakati mtu mwingine anapojaribu kuwadhulumu. Ukitaka kupata maongozi ya Mungu, soma vifungu vya Biblia vilivyoandikwa hapo chini, Sahihisha maneno yafuatayo yaliyoandikwa vibaya.



1 Petro 3:14b, 15

Mathayo 10:28

1 Petro 4:16

1 Wakorintho 16:13

Mathayo 5:44

1 Petro 3:14b, 15

Mtu ye yote akiniuliza juu ya imani yangu yanipasa kuwa tayari daima kumpa (BUJI) JIBU.

Mathayo 10:28

Hainipasi (KUWAOPAGO) KUWAO-GOPA wale wanaoua, wasiweze kuiua na roho.

1 Petro 4:16

Ikiwa ninateseka kwa sababu mimi ni Mkristo, hainipasi kuona (BIAU) AIBU.

1 Wakorintho 16:13

Mimi kama Mkristo, inanipasa kuwa macho, kusimama (IRAMA) IMARA katika imani, kufanya kiume na kuwa (HORIDA) HODARI.

Mathayo 5:44

Wakati mtu anapojaribu kuniudhi mimi, inanipasa (KUWANDAPE)

KUWAPENDA maadui zangu, (KUWABAKIRI) KUWABARIKI wale wanaonilaani, kuwatendea (MAME) MEMA wale wanaonichukia, na (KUWAOAMBE) KUWAO-MBEA wale wanaoniudhi.

Je! ni kwa nini Wakristo huchukiwa na watu ambao si Wakristo? Yesu anatupa sababu. (Yohana 15:18-20) Andika namba 1 kando ya sentensi iliyosemwa kwanza, na kuandika namba 2 kando ya sentensi iliyofuata, na kuendelea.

3 Ikiwa waliniudhi mimi, wata-
waudhi ninyi.

1 Mwajua ya kuwa ulimwengu
umenichukia mimi kabla ya
kuwachukia ninyi.

2 Naliwachagua katika ulimwe-
ngu.

Mtume Paulo alijaribu kumsaidia Timotheo Mkristo kijana kufahamu kwa nini Wakristo wanachukiwa na watu wasio Wakristo. (2 Timotheo 3:2, 3, 12) Andika namba 1 kando ya sentensi iliyosemwa kwanza, na kuandika namba 2 kando ya sentensi iliyofuata.

2 Wakristo wapendao kuishi
maisha ya utauwa katika
Kristo Yesu wataudhiwa.

1 Watu wa ulimwengu hujipenda
wenyewe na hawataki kumtii
Mungu.

Wakristo huteseka. Hata wakati mwingine wanauawa kwa sababu ya kuwa Wakristo. Je! hii inathibitisha kwamba hajali Wakristo? La. Kata

maneno yote yaliyo katika alama hii
() ambayo si kweli.

Paulo, Mkristo mkuu, aliteswa. Soma 2 Wakorintho 4:8,9. Paulo alisema, "Pande zote (twadhikika) (~~twafarajiwa~~), bali hatusongwi. (~~Tuneli-shwa-na-kuvalishwa~~) (Twaona shaka), bali hatukati tamaa. Twaudhiwa, bali (hatuachwi) (~~hatudhulumwi~~); twatupwa chini, bali (~~hatufi-moyo~~) (hatuangamizwi).

Katika Warumi 8:35-37 Paulo anauliza, "Ni nani- (~~atakayetupa~~) (atakayetutenga) na upendo wa Kristo? Je! ni (dhiki) (~~utajiri~~), au (shida) (~~mateso~~), au (adha) (~~afya~~), au (njaa) (~~kia~~) au (uchi) (~~umaskini~~), au (hatari), (~~bahati-mbaya~~), au (upanga) (~~kisu~~)? Lakini katika mambo hayo yote (tunashinda) (~~tunakufa-moyo~~), kwa yeye aliyetupenda.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?"

Waebrania 13:5b, 6

Je! unaweza kufikiria wakati unapomhitaji Bwana Yesu kuwa karibu nawe? Ona ya kwamba kuna sehemu tatu kwa vifungu hivi. Kila sehemu inakusaidia wakati unapokuwa taabuni. (Jaza nafasi zilizoachwa katika sehemu hizi.)

1. Alisema sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha.

2. Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye.

3. Mwanadamu atanitenda nini?

Rudia ahadi ya Mungu kila siku wakati unapoishi maisha pa kumpendeza Yesu. Kariri maneno hayo ili utaweza kuyakumbuka wakati wa taabu.



WAKATI WA KUFUNGA:

Wakumbushe wanafunzi maneno yaliyoandikwa kwenye ngao katika kazi yao ya kufanya. Mkate shauri pamoja jinsi wangeonyesha tabia yao kama wangemtegemea Bwana kuwasaidia kutii Neno lake. Kama kuna wakati zaidi, uwaruhusu wanafunzi kujadilia juu ya shida zinazoweza kuwakabili

kama wakisimama imara kwa ajili ya Kristo. Wakumbushe ya kwamba wakiogopa mapingamizi ya Shetani, ahadi za Mungu zilizo katika kifungu cha kukumbuka zitawasaidia. Watie moyo kusema vifungu hivyo kila siku.

Ombeni pamoja mpate nguvu ya kuishi kwa moyo wazi mbele ya Kristo na kutegemea ahadi zake wakati mnapokabiliwa na mapingamizi ya Shetani.

NJIA IMARA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 9:28-35;
Mathayo 17:5-9

KUJIANDAA KUFUNDISHA:

Wanafunzi wako sio mashujaa na wenye nguvu kama wanavyotamani kuonekana. *Kusudi la somo hili ni kuwasaidia kuona kwamba wakitaka kuonekana kuwa wenye nguvu wakati majaribu yanapowajia, ni lazima wamwamini Kristo sasa na kukua kila siku.* Wasaidie wanafunzi hao kufahamu ya kwamba kumweka Kristo kwanza maishani mwao ni jambo kubwa zaidi kuliko mambo ambayo wanafunzi wa Yesu walikuwa nayo wakati walipomwona Musa na Eliya mlimani.

MAMBO YA KUKAZA:

1. Yesu aliwatayarisha wanafunzi wake ili wangepanga kuwa na nguvu wakati ambapo imani yao ingejaribiwa.
2. Ni lazima tutegemee uwezo wa Mungu ili tuweze kuwa na nguvu.

KULIFUNDISHA SOMO:

(Uliza:) Je! mwalimu amekupa mtihani wa somo lo lote shuleni? Je! ulipenda kufanya mtihani huo? Kwa nini?

(Sema:) Ikiwa ulijitayarisha kwa mtihani huo ulifurahi kuufanya. Ikiwa hukujitayarisha, hukutaka kuufanya. Tukiwa tumekwisha kujitayarisha kwa jambo lo lote tunajisikia kuwa na nguvu.

Yesu alijua ya kwamba baada ya siku chache wanafunzi wake wangepabiliwa na majaribu ambayo yangeponyesha kama kweli wangepeshika mambo waliyoamini katika yeye. Jaribu lao lingetokea wakati ambapo Yesu, Masihi na Mfalme wao, angewaruhusu maadui zake kumsulibisha msalabani. Wakati ambapo jambo hili lingefanyika, Je! wangepuwa na shaka ya kwamba pengine Yesu hakuwa Masihi, mwana wa mungu? Je! wangesema, "Ikiwa Mungu anampenda Yesu, Mwanawe, kwa nini anamwacha kufa msalabani?" au "Kwa nini Yesu hawezi kutumia uwezo wake kuepuka kusulibiwa?"

Yesu alitaka kuhakikisha kwamba wanafunzi wake walikuwa tayari kwa jaribu hilo. Kama wangepuwa na kuwa na hakika kwamba Mungu ndiye aliyepanga hivyo, basi wangepuwa na nguvu ya kutosha kushinda majaribu.

Petro na Yakobo na Yohana, daima walipenda kutembea pamoja na Yesu. Mlima ulikuwa mrefu na wenye makokoto, na ilikuwa yapata saa nyingi usiku. Waliendelea kupanda mlima mpaka mwishowe Yesu akasimama kupumzika. Petro, Yakobo, na Yohana walipata mahali pa kuketi katikati ya miamba na mashina na Yesu akaenda upande mwingine kuomba. Walilemewa na usingizi, wakalala.

Wakati walipoamka, walionga jambo la kushangaza. Nuru kuu ilimulika. Nuru hiyo ilitoka kwa Yesu mwenyewe.

Uso wake uling'aa zaidi kuliko jua, na mavazi yake yalimetameta. Alionekana katika nuru ambayo haingeweza kutoka kwa kitu cho chote hapa duniani.

Mara mitume wale walipokuwa wakitazama, waliwaona watu wawili wakisimama pamoja na Yesu katika nuru hiyo. Ingawa Petro na Yakobo na Yohana hawakuwaona watu hao wawili wakati walipokuwa hai, walijua ya kwamba walikuwa watu wa Mungu walioishi zamani. Mmoja alikuwa Musa na mwingine alikuwa Eliya.



Sasa Yesu na Musa na Eliya walizungumza pamoja kuhusu wakati ambapo Yesu angekwenda Yerusalemu kukabili mauti. Bila shaka Yesu alieleza kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili ya dhambi za watu wote wa ulimwengu kulingana na mpango wa Mungu.

Wanafunzi walisikiliza kwa woga. Ingekuwaje kwamba yeye (Yesu) aliyekuwa na uzima wa milele angeweza kufa? Mpango huu ungekuwaje ukweli wa Mungu?

Je! wanafunzi wale walikuwa wakiota ndoto? La, walikuwa macho wakitetemeka kwa hofu iliyowashika. Wakati Musa na Eliya walipokuwa wakijitenga na Yesu, Petro alijaribu mara moja kuwazuia kuondoka. "Bwana mkubwa" Petro alisema, "ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu; kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya." (Luka 9:33) Petro aliwataka watu wale kutoka mbinguni kukaa nao kwa muda.

Lakini hata wakati Petro alipokuwa akisema, lilitokea wingu likawatia uvuli. Sauti ambayo haifanani na sauti yo yote ulimwenguni ilitoka katika wingu lile. Ilikuwa sauti ya Mungu mwenyewe aliyekuwa akisema kutoka katika wingu la utukufu wake. Alisema, "Huyu ni Mwanangu, mteule wangu, msikieni yeye." (Luka 9:35)

Wanafunzi walipoisia sauti ile, waliogopa sana wakaanguka kifudifudi. Walitetemeka kwa woga mpaka Yesu alipokuja na kuwagusa. Aliwaambia, "Inukeni, wala msiogope." Wanafunzi waliinua macho adhabu ya dhambi yako na ya dhambi yangu.

(Uliza:) Je! kwa kusikia sauti ya Mungu akisema kuliwasaidia wanafunzi kukabili majaribu yao?

(Sema:) Walipomsikia Mungu akimthibitisha Mwanawe kwao, walijua ya kwamba jambo lo lote ambalo Yesu alisema au alilofanya, alifanya kwa sababu alikuwa akimtii Baba yake.

yao lakini hawakuona mtu ye yote ila Yesu.

Baadaye, wakati walipoanza kushuka mlimani, Yesu aliwaonya. Aliwaambia "Msimwambie mtu ye yote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu." (Mathayo 17:9) Hawakuwaambia wanafunzi wengine wala viongozi wa dini.

Maajabu yote waliyoyaona na kuyasikia waliyaweza kuwa siri mioyoni mwao. Lakini waliulizana wao kwa wao, "Je! 'kufufuka katika wafu' maana yake nini?" Baadaye wangejua jibu wakati ambapo wangekabili majaribu ya kifo cha Yesu. Baadaye sana wangepata jibu la kuridhisha kwamba wangepata nguvu ya kukabili mauti wao wenyewe kwa mambo waliyoamini.

(Uliza:) Je! ni jambo gani lililofanyika mlimani mbalo lingewasaidia wanafunzi kuwa na nguvu katika imani yao wakati ambapo wangejaribiwa?

(Sema:) Waliona kwamba Yesu alikuwa Mungu. Utukufu wa Mungu ulionekana katika Yesu.

(Uliza:) Je! wanafunzi walipata msaada gani kwa kusikia mazungumzo ya Musa na Eliya juu ya kifo cha Yesu kilichotazamiwa kuja?

(Sema:) Baadaye mazungumzo hayo yaliwasaidia kutambua ya kwamba Yesu hakuwa tu Mwana wa Mungu bali pia alikuwa Mwokozi aliyekufa msalabani kuondoa adhabu ya dhambi ya kila mtu ulimwenguni - kuondoa

KAZI YA KUFANYA:

Soma kila swali na andiko la Biblia. Tafuta andiko la Biblia unajoweza kutumia kama msaada kwako. Kisha piga mstari chini ya jibu sawa la kila swali.



1. Kama Mungu alimpenda Yesu, kwa nini alimwacha kufa msalabani?

Soma Yohana 3:16.

Mungu alimwacha Yesu kufa kwa sababu anampenda kila mtu.

Yesu aliuawa kwa ajali.

2. Kama Yesu alijua kwamba usulubu ungekuwa mateso makuu, kwa nini hakukimbia ili kuwaeputa wale waliomchukia? Je! ilikuwa ni lazima Yesu kufa? Soma Yohana 10:17,18.

Yesu hangaliweza kukimbia kutoka kwa maadui zake.

Yesu alitoa uhai wake yeye mwenyewe na alikuwa na uwezo wa kuutwaa tena.

3. Ikiwa Yesu alijua kwamba angeishi tena, kwa nini hakukataa kusulibiwa na kuonyesha tu utukufu wake kwa kila mtu? Soma 2 Wakorintho 5:21 na 1 Petro 3:18.

Yesu alijiitoa mwenyewe kufa ili kuchukua lawama za dhambi zetu.

Yesu hangalithibitisha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu.

4. Je! ninapata wema gani nikiamini kwamba Yu hai sasa? Soma 2 Wakorintho 4:14 na Yohana 14:19.

Kwa sababu Yesu yu hai, tunajua ya kwamba Wakristo wataishi pia baada ya kufa.

Kwa sababu Yesu yu hai, tunafuma-
ini kuishi mpaka uzee wetu.

5. Naweza kuwa imara zaidi kuishi kama Mkristo? Soma Wafilipi 4:13.

Naweza kumtegemea Kristo kunitia nguvu ili niweze kushinda kila jaribu.

Naweza kufanya kazi kwa bidii na kutumainia kupita kila jaribu.

6. Je! inanipasa kufanya nini wakati ambapo nina taabu kubwa? Soma 1 Wakorintho 15:57, 58.

Nitafurahi ya kwamba nimeshinda jaribu na kutumainia kutokuwa na majaribu mengine.

Nitamshukuru Mungu kwa msaada wake wa kuniwezesha kushinda jaribu langu na kukabili majaribu mengine magumu zaidi.

Wanafunzi walipokuwa mlimani pamoja na Yesu walikuwa na mambo matatu muhimu yaliyowasaidia kuka-
bili majaribu yao, na yaliyowasaidia katika maisha yao. Je! mambo hayo matatu muhimu yalikuwa yapi?

1. Nuru ya Yesu.

2. Mazungumzo juu ya kifo cha Yesu kilichotazamiwa kuja kuonyesha njia ya msamaha wa dhambi.

3. Sauti ya Mungu kudhihirisha mpango wa Mungu.

Sisi hatuna nafasi kama ile ya kuona na kusikia mambo haya muhimu ambayo wanafunzi waliona na kusikia mlimani, lakini tuna mambo matatu ambayo yatakuwa ya msaada sana kwetu wakati tunapokabili majaribu maishani mwetu. Mambo haya pia yatatusaidia kila siku. Je! ni mambo gani?

1. Mwana wa Mungu aliye hai (Yupo pamoja nasi nyakati zote.)

2. Maombi (Tunaweza kusema na Yesu na kumsikiliza.)

3. Biblia (Tunamsikia Yesu akisema nasi kwa kitabu hiki.)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Kesheni, simameni imara katika imani, fanyeni kiume, mkawe hodari."

1 Wakorintho 16:13

Mungu anataka kukusaidia ili upate kushinda kila jaribu katika maisha yako. Hata hivyo, mara kwa mara wewe hukimbia majaribu magumu kwa sababu unaogopa. Kifungu hiki cha kukumbuka kitakuwa cha msaada hasa kwako kama utakitumia wakati utakapokihitaji.

Maongozi yetu kutoka kwa Yesu ni rahisi sana kuona. Yesu anajua ya kwamba tutakuwa na majaribu katika maisha yetu. Hii inatuonya kuwa macho; kusimama imara; kuwa na

nguvu. Tukifanya mambo haya, tutakuwa tayari kwa majaribu yote maishani mwetu na tunaweza kuwa na nguvu.



WAKATI WA KUFUNGA:

Wakati tunapofikiria kifungu chetu cha kukumbuka, tunaweza pia kufikiria Wafilipi 4:13 isemayo, “Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.” Je! ni mambo yapi mengine unayohitaji kufanya kama Mkristo? Na tuombe ombi hili, “Nayaweza _____

_____ katika Kristo anitiaye nguvu.” Je! ni uaminifu au utiifu kwa wazazi wako, au ni kumwamini Kristo kwa mambo yote? Katika kila jambo unamhitaji Kristo kukusaidia. Mwombe msaada katika ombi hili.